**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# DIRA 2050

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050

# (DIRA 2050)

© 2025 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Tume ya Taifa ya Mipango

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu yoyote ya chapisho hili inayoweza kunakiliwa kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya awali kutoka Tume ya Taifa ya Mipango, isipokuwa nukuu fupi kwa madhumuni ya kitaaluma, utafiti, au matumizi yasiyo ya kibiashara kwa kutaja chanzo ipasavyo.

**Nukuu Sahihi**
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2025). *Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050*. Dodoma; Tume ya Taifa ya Mipango.

**Kwa Mawasiliano**
Tume ya Taifa ya Mipango
S. L. P. 1324
Dodoma, Tanzania
Simu: 255 26 2961722
Baruapepe: es@planning.go.tz
Tovuti: www.planning.go.tz

# YALIYOMO

**YALIYOMO** ................................................................................. **iii**
**DIBAJI** ................................................................................. **v**
**UTANGULIZI** ................................................................................. **vii**

**1. MUKTADHA** ................................................................................. **1**

**2. DIRA** ................................................................................. **8**
2.1 Misingi ya Dira ................................................................................. 9
2.2 Malengo na Shabaha ................................................................................. 10
2.3 Muundo wa Dira ................................................................................. 11

**3. MSINGI MKUU WA DIRA** ................................................................................. **14**
**Utawala, Amani, Usalama na Utulivu** ................................................................................. **14**
3.1 Maeneo ya Kipaumbele ................................................................................. 15
3.1.1 Utawala Bora na Haki ................................................................................. 15
3.1.2 Serikali za Mitaa Imara na Zenye Ufanisi ................................................................................. 16
3.1.3 Utumishi wa Umma Unaowajibika ................................................................................. 17
3.1.4 Amani, Usalama na Utulivu ................................................................................. 18

**4. NGUZO ZA DIRA** ................................................................................. **20**
4.1 Nguzo ya Kwanza: Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani ................................................................................. 21
4.1.1 Uchumijumla Tulivu na Unaotabirika ................................................................................. 21
4.1.2 Mfumo Endelevu wa Kibajeti ................................................................................. 22
4.1.3 Vyanzo Anuai na Bunifu vya Mapato ................................................................................. 23
4.1.4 Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji ................................................................................. 25
4.1.5 Sekta Binafsi Imara ................................................................................. 26
4.1.6 Ushirikiano wa Kimkakati Kikanda na Kimataifa ................................................................................. 28
4.2 Nguzo ya Pili: Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii ................................................................................. 31
4.2.1 Jamii Iliyoelimika, yenye Ujuzi na Inayopenda Kujifunza ................................................................................. 31
4.2.2 Jamii yenye Afya ................................................................................. 33
4.2.3 Hifadhi ya Jamii ................................................................................. 34
4.2.4 Makazi Bora ya Gharama Nafuu ................................................................................. 36
4.2.5 Nguvukazi yenye Ujuzi na Ari ................................................................................. 37
4.2.6 Jamii yenye Umoja, Mshikamano na Inayowajibika ................................................................................. 38

4.3 Nguzo ya Tatu: Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ........ 41
4.3.1 Uhifadhi wa Bioanuai ........ 42
4.3.2 Uhifadhi wa Ardhioevu na Vyanzo vya Maji ........ 43
4.3.3 Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ........ 44
4.3.4 Usimamizi Madhubuti wa Ardhi ........ 45
4.3.5 Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ........ 46

**5. VICHOCHEO VYA KUFIKIA MALENGO YA DIRA ........ 49**
5.1 Usafirishaji Fungamanishi ........ 49
5.2 Nishati ........ 51
5.3 Sayansi na Teknolojia ........ 52
5.4 Utafiti na Maendeleo ........ 53
5.5 Mageuzi ya Kidijitali ........ 55

**6. SEKTA ZA MAGEUZI ........ 57**
6.1 Vigezo vya Uchaguzi wa Sekta ........ 58
6.2 Baadhi ya Sekta Zenye Fursa za Mageuzi kuelekea 2050 ........ 58

**7. MFUMO WA UTEKELEZAJI WA DIRA ........ 63**
7.1 Kuweka Vipaumbele Kimkakati ........ 63
7.2 Utekelezaji wa Dira ........ 64
7.3 Ushiriki wa Wadau ........ 64
7.4 Uratibu wa Utekelezaji ........ 64
7.5 Ufuatiliaji, Tathmini na Uwajibikaji ........ 64

**8. MWELEKEO ........ 66**

# DIBAJI



Ninayo furaha na wajibu wa kuwasilisha kwenu Watanzania wenzangu Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 – Dira 2050. Huu ni mpango thabiti, jumuishi na wenye maono ya mbali, unaoakisi matarajio yetu ya pamoja na mwelekeo wa kimkakati kwa kipindi cha miaka ishirini na mitano ijayo.

Tangu Tanzania Bara ilipopata uhuru mwaka 1961, Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 na Muungano wa kihistoria uliounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Aprili 1964, tumeelekeza jitihada zetu zote kwenye kutokomeza ujinga, maradhi na umaskini na kuinua hali ya maisha ya watu wetu. Mwaka 2000, tulizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 – Dira 2025, ikiwa ni mwongozo wetu wa kwanza wa muda mrefu wa maendeleo ya taifa letu. Dira hii ililenga kuibadilisha nchi yetu kutoka uchumi wa kilimo wenye tija ndogo hadi kufikia uchumi wa kipato cha kati unaochochewa na viwanda na unaozingatia maendeleo ya watu kama msingi wa ustawi wa taifa.

Utekelezaji wa Dira 2025 ulikuwa wa mafaniko makubwa. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuongezeka kwa kipato cha wastani cha kila Mtanzania takribani mara tatu, kutoka dola za Marekani 453 mwaka 2000 hadi dola 1,277 mwaka 2023. Vilevile, umri wa kuishi uliongezeka kutoka wastani wa miaka 51 mwaka 2000 hadi miaka 68 mwaka 2024. Tuliongeza fursa za upatikanaji wa elimu, huduma za afya, maji safi na salama, pamoja na ustawi wa jamii. Kutokana na umoja, mshikamano wa kitaifa pamoja na nia thabiti, Tanzania imeendelea kuwa nchi ya amani na utulivu, sifa ambazo ndiyo msingi wa mafanikio yetu.

Pamoja na mafanikio haya, ni dhahiri kuwa dunia inayotuzunguka inabadilika kwa kasi kubwa zaidi kuliko wakati mwingine wowote. Mabadiliko haya yanachochewa na mienendo mipya ya kimataifa, mageuzi makubwa ya teknolojia na matarajio makubwa ya kizazi kipya chenye maarifa, nguvu, uthubutu na ari ya mabadiliko. Katika muktadha huu, imetulazimu kuwa na dira mpya na yenye malengo makubwa na ya muda mrefu kwa ajili ya nchi yetu.

Dira 2050 inaweka bayana azma yetu ya kuifikisha Tanzania kwenye ngazi ya juu ya maendeleo, yaani kuwa nchi yenye uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu utakaongozwa na maarifa na maendeleo ya viwanda.

Matarajio yetu ni kwamba, ifikapo mwaka 2050, pato la taifa litakuwa lenye thamani ya dola za Marekani trilioni moja na wastani wa pato la mtu mmoja litakuwa na thamani ya dola za Marekani 7,000 kwa mwaka.

Dira 2050 imejengwa juu ya msingi madhubuti wa utawala bora, amani, usalama na utulivu ambavyo ni nguzo muhimu katika kuyafikia malengo yetu. Katika kuendeleza msingi huu, tunatambua na kuheshimu utu wa kila mtu, pamoja na kuthamini mchango wa nafasi ya kila mmoja katika jamii. Tunasimamia kwa dhati demokrasia na utawala wa sheria, huku tukilinda haki na uhuru wa msingi wa kila raia. Amani na umoja wetu ndiyo mhimili wa mshikamano wa kitaifa na ulinzi wa uhuru wetu. Kwa kutambua wajibu wetu kwa vizazi vijavyo, tunalinda na kusimamia utajiri wa rasilimali kwa manufaa ya sasa na baadaye. Vilevile, tunaenzi na kuendeleza urithi wa utamaduni wetu ambao umejenga utambulisho wa taifa letu na kuimarisha umoja na mshikamano.

Ni muhimu kutambua kuwa Dira 2050 siyo mpango wa serikali pekee, bali ni mpango wa kitaifa unaotokana na maoni na matarajio ya wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo. Kwa msingi huo, Dira 2050 inaakisi matarajio ya pamoja kuhusu mustakabali wetu na namna ya kuyafikia matarajio hayo.

Ili kutimiza malengo ya Dira 2050, ni lazima tujenge utamaduni wa utekelezaji na uwajibikaji, pamoja na kuzingatia weledi na ubunifu katika utendaji wetu. Hivyo, natoa rai kwa wizara zote, taasisi za umma, sekta binafsi, asasi za kiraia, wadau wa maendeleo, vyama vya ushirika na makundi ya kijamii kuhakikisha kuwa sera, mipango na mikakati ya kisekta zinafungamanishwa na malengo ya Dira hii.

Kwa pamoja, tusonge mbele ili kuijenga Tanzania kuwa taifa jumuishi, lenye ustawi, haki na linalojitegemea; na kuendelea kuwa taifa linaloheshimika duniani.

..............................................................................

Dkt. Samia Suluhu Hassan

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

*17 Julai 2025*

# UTANGULIZI



Tanzania inatarajiwa kukamilisha rasmi utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ifikapo Juni 2026. Kwa kuzingatia Kifungu cha 6(2)(b) cha Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango ya mwaka 2023, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliiagiza Tume ya Taifa ya Mipango kuandaa dira mpya itakayotoa mwelekeo wa safari ya maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka ishirini na tano ijayo. Kufuatia agizo hilo, mchakato wa kuandaa Dira 2050 - ulianza rasmi Aprili 2023.

Ili kuhakikisha kuwa dira mpya inabeba maono ya Watanzania, tarehe 9 Desemba 2023, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo kuhusu Dira 2050. Timu ya wataalamu iliratibu maoni ya wadau kutoka makundi mbalimbali, wakiwemo viongozi wa serikali, asasi za kiraia, wadau wa maendeleo, viongozi wa dini, wanafunzi na wananchi kwa ujumla. Njia mbalimbali zilitumika kukusanya maoni, ikiwemo tafiti za kaya, mahojiano kwa njia ya simu, mifumo ya kidijitali, ujumbe mfupi wa simu ya mkononi, semina na makongamano.

Kwa kuzingatia maoni ya wananchi na wadau, historia na uzoefu wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya awali, pamoja na uzoefu wa nchi nyingine zilizopiga hatua kubwa kimaendeleo, timu ya wataalamu iliandaa Rasimu ya Kwanza ya Dira 2050. Rasimu hiyo ilizinduliwa Zanzibar, tarehe 11 Desemba 2024 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, uzinduzi wa Rasimu ya Dira ulikwenda sambamba na uzinduzi wa awamu ya pili ya kukusanya maoni ya wadau yaliyolenga kuboresha maudhui ya Rasimu hiyo ili kuhakikisha kuwa inaakisi matarajio ya pamoja ya Watanzania.

Baada ya mchakato shirikishi wa awamu ya pili ya ukusanyaji wa maoni, Timu ya Wataalam ilitoa rasimu ya mwisho ya Dira Machi 2025. Hatua iliyofuata ilihusisha uchambuzi wa kina wa Rasimu hiyo ndani ya vyombo vya maamuzi vya Serikali. Tarehe 22 Juni 2025, Baraza la Mawaziri liliidhinisha rasmi Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, kwa kifupi Dira 2050. Dira 2050 iliwasilishwa na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Juni 2025.

Msingi Mkuu wa Dira 2050 ni utawala bora, amani, usalama na utulivu. Dira hii inajengwa na nguzo kuu tatu zinazoshabihiana kama ifuatavyo:

1. *Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani:* Nguzo hii inalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu kwa kuimarisha uwezo wa kifedha, kuchochea ukuaji wa vyanzo bunifu vya ugharamiaji, na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

2. *Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii:* Nguzo hii inalenga kujenga rasilimali watu yenye ujuzi, maisha yenye staha, usawa na utu kwa Watanzania, wanaotarajiwa kufikia zaidi ya milioni 118 ifikapo mwaka 2050. Lengo hili linatarajiwa kufikiwa kupitia malezi na makuzi bora ya watoto, elimu na mafunzo bora, huduma bora za afya kwa wote, nishati safi, pamoja na mifumo jumuishi na thabiti ya hifadhi ya jamii. Nguzo hii inadhihirisha dhamira ya taifa ya kujenga jamii jumuishi, inayozingatia usawa wa kijinsia, mshikamano wa kitaifa na kupunguza tofauti za kimaendeleo kati ya mikoa na makundi ya kijamii.

3. *Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi:* Nguzo hii inalenga kuifanya Tanzania kuwa kinara kimataifa katika uhifadhi wa mazingira kwa kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za asili na kuimarisha uwezo wa Taifa wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Ili kufanikisha malengo haya, Dira 2050 imeainisha vichocheo vitano vya kimkakati vya mabadiliko:

1. *Usafirishaji Fungamanishi:* Azma kubwa ni kuitumia vyema nafasi ya kipekee ya Tanzania kijiografia ili kuijenga kuwa kitovu cha biashara na usafirishaji kikanda kupitia uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya kisasa, mifumo ya biashara ya kidijitali, na kuimarisha ushirikiano wa kikanda.

2. *Nishati:* Kujenga mfumo bora wa nishati safi ulio nafuu na wa kuaminika ili kuchochea mageuzi ya kijamii na kiuchumi. Lengo la muda mrefu ni kuifanya Tanzania kuwa muuzaji mkuu wa nishati nje ya nchi ifikapo mwaka 2050.

3. *Sayansi na Teknolojia*: Kuongeza uzalishaji na ukuaji wa uchumi kupitia matumizi ya teknolojia bunifu, kuimarisha ekolojia ya mifumo ya uvumbuzi na upatikanaji jumuishi wa teknolojia ya kidijitali.


4. *Utafiti na Maendeleo:* Kuimarisha mfumo wa uvumbuzi kwa kuchochea ongezeko la uwekezaji angalau kufikia asilimia moja ya pato la Taifa, kukuza ushirikiano baina ya taasisi za elimu ya juu na sekta ya viwanda, pamoja na kuhakikisha ulinzi madhubuti wa haki miliki.

5. *Mageuzi ya Kidijitali:* Kupanua uelewa wa matumizi ya teknolojia ya kidijitali na kuimarisha upatikana wake ili kuongeza ufanisi wa Serikali, kuwezesha uchakataji wa takwimu kibiashara na kuhakikisha usimamizi wa mifumo ya kidijitali unaozingatia maadili.

Ili kuelekeza vyema jitihada za utekelezaji na uwekezaji, Dira 2050 imeweka mfumo wa kutambua sekta za kipaumbele kwa kuzingatia vigezo vitano: uwezo wa kuzalisha ajira, kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi, kuwa na uhusiano baina ya sekta, uwezo wa kuongeza thamani katika bidhaa na mapato ya Serikali. Vigezo hivi vitaiwezesha Tanzania kutumia kikamilifu fursa ilizonazo kwa maendeleo endelevu.

Fursa iliyopo mbele yetu ni kubwa. Kwa idadi ya watu inayokadiriwa kufikia zaidi ya milioni 118 ifikapo mwaka 2050, wengi wao wakiwa ni vijana, Tanzania ina uwezo wa kujenga uchumi wenye thamani ya dola za Marekani trilioni moja. Uchumi huu utaleta matokeo chanya katika maisha ya watu, kwa kuboresha ustawi wa familia na kuimarisha maendeleo ya jamii.

Ninatoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunipa heshima ya kuongoza mchakato muhimu wa maandalizi ya Dira 2050. Nina matumaini makubwa kuwa Dira hii itakuwa mwongozo muhimu wa mipango ya maendeleo ya nchi yetu, katika kipindi cha robo karne ijayo.



Prof. Kitila Alexander Mkumbo

***Waziri wa Nchi***

***Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji***

*17 Julai 2025*

# 1. MUKTADHA

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi moja inayoundwa na Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, ikiwa na ukubwa wa eneo la kilomita za mraba ($km^2$) 948,740, zikiwemo $km^2$ 61,500 za maziwa na mito. Tanzania ipo katika ukanda wa Afrika ya Mashariki, katika ukanda wa Maziwa Makuu ikipakana na Kenya na Uganda kwa upande wa kaskazini; Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa upande wa magharibi; Zambia, Malawi na Msumbiji kwa upande wa kusini; na Bahari ya Hindi kwa upande wa mashariki. Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, ilionesha kuwa Tanzania ina watu milioni 61.7, na hivyo kuwa miongoni mwa nchi zenye idadi kubwa ya watu barani Afrika. Aidha, kwa mujibu wa sensa hiyo, asilimia 43 ya watu wote walikuwa na umri usiozidi miaka 15, kiwango kinachozidi wastani wa nchi za bara la Afrika ambao ni asilimia 41.

Tanzania inasifika kwa utajiri wake wa tamaduni, mila na desturi mbalimbali pamoja na ukarimu kwa wageni. Ikiwa ni makazi ya zaidi ya makabila 120, urithi wa utamaduni wake unaonekana kupitia muziki wenye vionjo na midundo hai, ngoma, sanaa na desturi zinazounganisha jamii. Kiswahili kama lugha ya taifa, imekuwa nyenzo muhimu ya kukuza mshikamano, umoja na utambulisho wa taifa. Desturi ya ukarimu imeipa Tanzania sifa kama nchi yenye amani na utulivu inayokaribisha wageni, na hivyo kuweka msingi thabiti wa maendeleo endelevu.

Vilevile, Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye utajiri mkubwa wa maliasili, mabonde makubwa na ardhi yenye rutuba. Nchi hii ina vivutio mashuhuri vya utalii duniani, ikiwa ni pamoja na Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Serengeti, magofu ya kihistoria ya Kilwa, fukwe za kuvutia na visiwa vya Zanzibar. Zaidi ya vivutio hivi vya asili, Tanzania ni kitovu muhimu cha historia ya mwanadamu, ambapo Bonde la Olduvai ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro ni ushahidi wa urithi wa pamoja wa asili ya binadamu, likihifadhi mabaki ya baadhi ya watu wa kale yaliyokadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka milioni 1.8 na milioni 2.1.

## Safari ya Maendeleo Baada ya Uhuru

Mwaka 2024 Tanzania iliadhimisha miaka 60 tangu kuasisiwa kwake, kufuatia kuungana kwa nchi mbili zilizokuwa huru, Tanganyika na Zanzibar. Tukio hili muhimu linaakisi miongo sita ya maendeleo thabiti na himilivu, kuanzia uhuru wa Tanganyika mwaka 1961, na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Safari ya Tanzania ya kuwa taifa huru iliongozwa na dhamira ya dhati ya kujenga usawa, udugu na uhuru, chini ya uongozi mahiri wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa kwanza wa Tanganyika na Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Viongozi hawa walijenga mshikamano na kuondoa tofauti za kikabila, kitamaduni na kidini. Maono haya ya umoja yalizidi kuimarika kufuatia uamuzi wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa, hatua iliyoleta utambulisho wa pamoja na kudumisha mshikamano wa kijamii.

Sera za awali za maendeleo zililenga kupambana na maadui watatu wa maendeleo ambao ni umaskini, ujinga na maradhi. Katika sera hizi, serikali iliweka msisitizo katika kujenga jamii shirikishi kwa kutoa elimu na huduma za afya kwa wote, sambamba na kuanzisha mipango ya maendeleo ya jamii. Mnamo mwaka 1967, Tanzania ilitangaza Azimio la Arusha lililotoa mwelekeo wa uchumi na maendeleo kwa kufuata misingi ya Ujamaa na Kujitegemea. Azimio la Arusha liliweka nguzo ya mshikamano wa kitaifa uliojengwa juu ya misingi ya usawa, uadilifu, haki, mshikamano na kujitegemea. Katika kipindi cha utekelezaji wake, Tanzania ilipata mafanikio makubwa katika kupanua huduma za afya, elimu, maji na usafi wa mazingira, nishati na maendeleo vijijini.

Katikati ya miaka ya 1970, Tanzania ilikumbwa na changamoto kubwa za kimaendeleo. Kwa upande mmoja, utekelezaji wa sera za Ujamaa kwa lengo la kujenga uchumi unaojitegemea kupitia uhamasishaji wa vijiji na kilimo kilichohodhiwa na serikali, ulianza kudorora. Hii ilitokana na usimamizi hafifu, ukosefu wa miundombinu na uzalishaji mdogo kwenye sekta ya kilimo, hali iliyosababisha vijiji vingi kushindwa kujiendeleza na kusababisha uhaba mkubwa wa chakula. Kwa upande mwingine, kuporomoka kwa mapato ya mauzo ya nje yatokanayo na mazao ya biashara kama vile kahawa, pamba na mkonge, kuliifanya nchi ianze kutegemea zaidi mikopo ya kigeni.

Aidha, katika kipindi hiki, Tanzania ilikumbwa na mdororo mkubwa wa kiuchumi uliosababishwa na kuyumba kwa uchumi wa dunia, na vita vya Kagera dhidi ya utawala wa kifashisti wa nduli Idi Amin nchini Uganda (1978 –1979). Vita hiyo iliongeza mzigo kwenye bajeti ya Taifa, ambapo Serikali ililazimika kuelekeza rasilimali nyingi kwenye sekta ya ulinzi badala ya maendeleo. Wakati huo huo, mgogoro wa mafuta wa dunia katika miaka ya 1970 ulisababisha kupanda kwa gharama za uagizaji bidhaa, hali iliyochochea mfumuko wa bei na kudhoofisha zaidi uchumi mchanga wa Tanzania. Kufikia miaka ya 1980, deni la Taifa lilizidi kuongezeka sambamba na kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni, hali iliyofanya uchumi kuzidi kuzorota.

Wakati ikiendelea kukabiliana na hali hiyo, Tanzania ilishinikizwa kutekeleza mageuzi ya kiuchumi kutoka Shirika la Fedha Duniani na Benki ya Dunia. Katikati ya miaka ya 1980, yalifanyika mabadiliko makubwa ambapo Tanzania ililazimika kuingia kwenye mfumo wa soko huria. Katika mazingira haya, mashirika ya umma yalibinafsishwa, hatua zikachukuliwa kuweka mazingira bora zaidi ya ukuaji wa sekta binafsi na kupunguza usimamizi wa serikali katika uchumi. Mageuzi haya yalibadili kwa kiasi kikubwa mwelekeo wa kiuchumi na ikawa mwanzo wa kujifungamanisha na mifumo ya soko huria. Pamoja na hatua hizi kuonekana kama ndiyo ingekuwa dawa ya matatizo ya kiuchumi ya wakati huo, zilijitokeza changamoto nyingine nyingi za kijamii na kiuchumi.

Mabadiliko yaliyofanyika katika sera za uchumi yaliambatana na mageuzi ya kisiasa, ikiwa ni pamoja na kurejea kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka

1992, na hivyo kufungua ukurasa mpya katika siasa za Tanzania. Jambo hili lilikuza demokrasia, ushirikishwaji wa kisiasa wa wananchi na kuimarisha asasi za kiraia. Juhudi hizi ziliweka msingi wa kuhamasisha ushiriki mkubwa zaidi wa wananchi katika masuala ya utawala.

Katika medani za kimataifa, Tanzania imekuwa nguzo muhimu ya harakati za ukombozi wa Bara la Afrika, ikijulikana kwa kuhimiza na kuchangia kuwepo kwa amani, utulivu na mshikamano wa kikanda. Chini ya uongozi mahiri wa Mwalimu Julius K. Nyerere, Tanzania ilitoa hifadhi na mafunzo kwa wapigania uhuru waliopambana dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi Kusini mwa Afrika.

Kwa kuzingatia hadhi yake katika harakati za ukombozi, Tanzania imekuwa muhimili katika kuleta muafaka wa siasa za kikanda. Jiji la Dar es Salaam limekuwa kitovu na alama ya mshikamano baina ya nchi za Afrika, likiashiria jukumu muhimu la Tanzania katika mapambano dhidi ya ukoloni. Kadhalika, Tanzania imeendelea kuwa mshirika mkuu katika usuluhishi wa migogoro katika nchi jirani na kuchangia juhudi za ujenzi wa amani katika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Pamoja na kuongoza harakati za ukombozi, Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda, ikichangia kwa kiasi kikubwa kuanzishwa kwa jumuiya za kikanda kama Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. Kupitia jumuiya hizi, Tanzania imeshiriki kukuza ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara na kuendeleza miundombinu ya kikanda, ikiwemo usafirishaji na nishati.

Kama mwanachama wa Umoja wa Afrika na mtetezi imara wa ushirikiano wa nchi zinazoendelea ulimwenguni (*South-South Cooperation*), Tanzania imekuwa mstari wa mbele kutatua migogoro, kutetea haki za binadamu na kuchangia maendeleo endelevu. Ukarimu wake wa kuwahifadhi mamilioni ya wakimbizi unaakisi azma yake isiyoyumba ya kuendeleza utulivu wa kikanda, ustawi wa pamoja na mustakabali endelevu kwa Afrika.

## Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Katika kujiwekea mipango thabiti ya maendeleo, mwaka 2000 Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambayo ililenga kulijenga taifa kuwa nchi ya kipato cha kati. Maeneo ya kipaumbele yalikuwa ni kilimo cha kisasa, viwanda, miundombinu na teknolojia. Dira 2025 imeleta mabadiliko makubwa katika maisha ya watu, ukuaji wa uchumi, na utawala, huku kukiwa na ongezeko la ushiriki wa wanawake katika siasa na uchumi.

Tangu kuzinduliwa mwaka 2000, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 imekuwa nyenzo muhimu katika kusukuma mbele maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini Tanzania. Msingi wa mafanikio haya umejengwa juu ya misingi ya amani, utulivu na umoja wa kitaifa, hali iliyowezesha utekelezaji wa sera, kuvutia uwekezaji, na kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

Katika nyanja za kiuchumi, Tanzania ilidumisha kasi ya ukuaji endelevu, ambapo pato halisi la taifa liliongezeka kwa wastani wa asilimia 6.2 kwa mwaka kati ya mwaka 2000 na 2024. Mfumuko wa bei ulidhibitiwa na kuendelea kubaki ndani ya lengo la tarakimu moja, hatua iliyosaidia kuleta utulivu wa uchumi na kuongeza uwezo wa wananchi kumudu gharama za maisha. Wakati huohuo, pato la mtu mmoja lilikua na kufikia wastani wa dola za Marekani 453 mwaka 2000 hadi dola 1,277, mwaka 2023. Vilevile, kiwango cha umasikini uliokithiri kilipungua kutoka asilimia 36 mwaka 2000 hadi asilimia 26 mwaka 2024. Mafanikio haya yaliiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati cha chini mwezi Julai 2020.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni: kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 51 mwaka 2000 hadi miaka 68 mwaka 2024; kupungua kwa vifo vinavyotokana na uzazi kutoka 750 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2000 hadi 104 mwaka 2022. Upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka asilimia 32 vijijini na asilimia 55 mijini mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 79.9 vijijini na asilimia 94 mijini mwaka 2024. Katika elimu, uandikishaji wa watoto shule za msingi umefikia asilimia 98 mwaka 2024, sambamba na ongezeko kubwa la wanaojiunga na elimu ya sekondari. Aidha, jitihada za kupambana na rushwa zimeimarika, na ukuaji wa sekta ya viwanda umechangia kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi kutoka dola milioni 43.1 mwaka 2000 hadi dola bilioni 1.4 mwaka 2024. Kwa ujumla, utekelezaji wa Dira 2025 umeimarisha msingi wa maendeleo ya watu, uchumi wa taifa na mwelekeo wa ustawi jumuishi unaozingatia maslahi ya Watanzania wote.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, Tanzania haikufanikisha kikamilifu malengo yote ya Dira 2025. Ingawa nchi ilifikia hadhi ya uchumi wa kipato cha kati ngazi ya chini na pato la mtu mmoja liliongezeka, haikufikia lengo la kuwa na wastani wa pato la mtu mmoja wa dola za Marekani 3,000 kwa mwaka. Vilevile, licha ya ukuaji wa uchumi wa kiwango cha kuridhisha, maendeleo hayakujumuisha ipasavyo wananchi wote, wala kuleta manufaa kwa usawa. Kasi ya ukuaji wa uchumi haikwenda sambamba na matarajio ya kupunguza umasikini kwa kiwango kilichohitajika. Idadi kubwa ya wananchi, hususan wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, bado wameendelea kujikimu kupitia sekta isiyo rasmi, hali inayowakosesha fursa stahiki za kiuchumi na kijamii.

Kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kulichangiwa na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mdororo wa uchumi wa dunia mwaka 2008; migogoro ya kisiasa na kiuchumi katika mataifa mbalimbali; athari za mabadiliko ya tabianchi; janga la UVIKO 19; na mabadiliko ya sera za nchi washirika wa maendeleo. Aidha, mabadiliko ya mara kwa mara ya sera na miundo ya taasisi yalichangia ukosefu wa utulivu katika miongozo ya serikali na kudhoofisha utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo. Changamoto nyingine ni pamoja na uhaba wa fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Dira; na kutokuwepo kwa mpango elekezi wa muda mrefu kwa miaka kumi ya awali ya utekelezaji wa Dira 2025. Sababu nyingine

ni pamoja na: elimu na ujuzi usiokidhi mahitaji ya soko la ajira; kutokutumia kikamilifu fursa za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika shughuli za kijamii na kiuchumi; miundombinu duni na mipangomiji isiyokidhi mahitaji; utegemezi wa vyanzo vya nishati visivyo na uhakika; na kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ya kilimo ambayo imeendelea kukua chini ya asilimia 4, hali iliyoathiri jitihada za kupunguza umasikini wa watu waishio vijijini kwa kiwango stahiki.

Dira 2025 inatarajiwa kukamilika rasmi mwezi Juni 2026. Kufuatia ukomo huu na mabadiliko ya kasi ya kiuchumi na kijamii duniani, na maendeleo ya kiteknolojia, kuna haja ya kuandaa Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo itakayoendeleza mafanikio ya Dira 2025 na itakayoendana na mabadiliko ili kutoa mwelekeo wa maendeleo ya nchi. Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 6(2)(b) cha Sheria ya Tume ya Mipango ya Mwaka 2023, Tume ya Taifa ya Mipango inawajibika kuandaa dira ya taifa ya maendeleo pamoja na mipango ya maendeleo ya muda mrefu, ya kati na ya muda mfupi, na pia kuhakikisha usimamizi wa utekelezaji wake kwa ufanisi.

## Tanzania ya Mwaka 2050

Ifikapo mwaka 2050, Tanzania itakuwa nchi ya mfano katika ustahimilivu, ubunifu, ustawi na diplomasia barani Afrika na duniani, ikichochewa na rasilimali zake, miundombinu imara na nguvukazi mahiri na yenye motisha. Inatarajiwa kuwa nchi yenye kipato cha kati ngazi ya juu, ikiwa na pato la taifa lenye thamani ya dola za Marekani trilioni moja na wastani wa pato la mtu mmoja lenye thamani ya dola za Marekani 7,000 kwa mwaka. Uchumi wake utakuwa shindani na mseto, unaotegemea viwanda na ukichagizwa na nguvukazi yenye maarifa na ujuzi.

Ili kufanikisha Dira hii, yanahitajika mabadiliko ya haraka na ya kina, yakiwemo mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara, kilimo chenye tija zaidi, umeme wa uhakika, kuendeleza ujenzi mkubwa zaidi wa miundombinu ya kisasa, nguvukazi yenye ujuzi na mageuzi ya kidijitali ya kiwango cha juu. Kijiografia, Tanzania ipo katika eneo la kimkakati na ina nafasi nzuri ya kuwa kitovu cha biashara ya usafirishaji na kufikia masoko ya kikanda. Vilevile, Tanzania inabaki kuwa miongoni mwa nchi zenye amani na utulivu barani Afrika, ikiwa na uzoefu wa kujenga umoja wa kitaifa na maelewano bila kujali tofauti za kidini, kisiasa, kikabila, kijinsia au kikanda.

Katika muktadha huu, dhamira kuu ni kujenga taifa lenye nguvukazi iliyoelimika, yenye ujuzi na maono, ambayo itafanikisha maendeleo endelevu. Nguvukazi hii itajengwa katika misingi ya ubunifu, ujasiriamali na uwajibikaji. Kwa kutambua kwamba wanawake na vijana ni sehemu kubwa ya idadi ya watu na ni nguzo muhimu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, Dira 2050 inaweka kipaumbele cha ushiriki wa makundi haya katika maendeleo, kwa kutumia vipaji, uwezo na ari yao katika kufanikisha ukuaji wa kiuchumi na maendeleo jumuishi.

Sekta binafsi ina nafasi kubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hivyo Dira 2050 inalenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kuiwezesha sekta hiyo kuwa imara na shirikishi ili kuendeleza uvumbuzi, ubunifu na ukuaji endelevu. Dira hii pia inalenga kufanya mabadiliko na mageuzi makubwa katika sekta binafsi huku ikitoa fursa sawa za kiuchumi kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kwa kuzingatia mafanikio na uzoefu uliopatikana kutoka Dira 2025, Dira 2050 inalenga kuiwezesha Tanzania kutumia rasilimali zake kikamilifu ili kujiletea maendeleo na hivyo kuwa taifa lenye nguvu kiuchumi barani Afrika na kwingineko.

Ifikapo mwaka 2050, Tanzania inalenga kuendelea kuongoza kikanda na kimataifa kupitia utekelezaji wa sera yake ya mambo ya nje, hususan masuala ya ulinzi, usalama na amani. Kama mpatanishi wa kuaminika na kupitia ushiriki wake katika michakato ya amani katika Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania itaimarisha ushawishi wake wa kidiplomasia na kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi. Dhamira yake ya kudumisha amani itachochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kuvutia uwekezaji wa kimataifa na kuchangia ustawi wa maendeleo ya Bara la Afrika na dunia kwa ujumla.

Kuelekea mwaka 2050, Tanzania itakumbana na mabadiliko makubwa ya kijamii, kiuchumi na kimazingira. Mabadiliko hayo ni pamoja na ongezeko la kasi ya ukuaji wa miji, mabadiliko ya muundo wa idadi ya watu kwa mujibu wa rika, athari za mabadiliko ya tabianchi, kuibuka kwa teknolojia bunifu zinazobadili kwa haraka mazingira ya maisha na biashara, pamoja na mivutano ya kijiopolitiki katika ngazi ya kimataifa. Mabadiliko haya yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa mwelekeo wa maendeleo ya taifa.

Mabadiliko katika muundo wa idadi ya watu kiumri yataleta changamoto mbili kuu, kwa upande mmoja, kuongezeka kwa idadi ya wazee kutasababisha upungufu wa nguvukazi; kwa upande mwingine, idadi kubwa ya vijana itaongeza mahitaji ya ajira mpya. Kwa kuwa Tanzania ina idadi kubwa ya vijana, na ikizingatiwa mchango wao katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kuna haja ya kuweka mikakati madhubuti ya kuwaendeleza na kutumia ipasavyo rasilimali hiyo.

Kutokana na ukuaji miji na maendeleo ya kiteknolojia, Tanzania itahitaji ubunifu wa hali ya juu ili kujenga ujuzi, kuwa na mipango miji endelevu na matumizi sahihi ya teknolojia. Mivutano ya kijiopolitiki itakayotokana na utaifa na kugombania rasilimali, itachagiza kuwepo kwa mfumo mpya wa kujenga amani na ushirikiano wa kimataifa. Hivyo, itakuwa muhimu kuimarisha uhusiano kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea, pamoja na kuendeleza ushirikiano wa kikanda katika masuala ya kiuchumi, kama vile jumuiya iliyoanzishwa na nchi za Brazili, Urusi, India, China, na Afrika ya Kusini (BRICS).

Wakati huo huo, usalama mitandaoni utakuwa hatarini kutokana na ongezeko la matumizi ya akili unde na upotoshaji wa taarifa mitandaoni. Hali hii itaongeza tabaka jipya la changamoto, na hivyo itahitajika mikakati thabiti ya kuweka uwiano kati ya ulinzi wa maslahi ya nchi na matumizi ya fursa chanya zitokanazo na mageuzi ya kasi ya kiteknolojia. Pamoja na changamoto hizi zitakazokuwa na taathira kwa maendeleo ya jamii, itakuwa ni fursa ya pekee ya kuachana na mitindo kazi ya zamani ili kuzingatia teknolojia za kijani na kuanzisha biashara, viwanda na sekta mpya shindani.

Tanzania itakuwa na uwezo mkubwa wa kukabiliana na changamoto zozote za kimaendeleo, kwa kuweka mipango himilivu, kuwa na mikakati ya kuangalia mbele na kufanya mabadiliko makubwa ya kimtazamo. Itaweza pia kutumia fursa zitakazojitokeza kuchochea maendeleo endelevu jumuishi na yenye usawa. Vilevile, Tanzania itanufaika na nguvukazi ya vijana na utajiri wake wa asili, huku ikitumia nyenzo hizo kuchangia malengo endelevu ya dunia na kukuza ustawi wa nchi.

# 2. DIRA

## *Taifa Jumuishi Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea*

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inaanzisha safari ya mabadiliko makubwa, ili ifikapo katikati ya karne ya 21 Tanzania iwe Taifa lenye ustawi, usawa na uwezo wa kujitegemea. Msingi wa Dira hii ni maendeleo ya watu yanayochochewa na uchumi imara, wenye ushindani na kipato cha juu, ili kuinua viwango vya maisha ya wananchi na kuondoa umasikini. Kufikia mwaka 2050, Tanzania inalenga kuwa kitovu cha viwanda katika ukanda wa mashariki na kusini mwa Afrika, ikiwa na uchumi jumuishi na shindani, unaostahimili misukosuko. Taifa hili litakuwa na nguvukazi yenye ujuzi wa hali ya juu, jamii inayothamini na kuhifadhi mazingira, inayozingatia misingi ya usawa wa kijamii, ustawi kwa wote na maendeleo endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Dira 2050 hii imejengwa juu ya msingi wa historia ya maendeleo ya taifa katika miongo iliyopita, sambamba na mafanikio yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa Dira 2025, hususan katika mapambano dhidi ya umaskini, maradhi na ujinga. Mafanikio haya yameweka msingi thabiti wa kuandaa mwelekeo wa baadaye wa maendeleo ya nchi, kwa kuzingatia mahitaji na fursa mbalimbali. Kwa kuzingatia historia yake ya amani na utulivu, nafasi ya kimkakati kijiografia, utajiri wa maliasili na maendeleo ya sayansi na teknolojia, hususan teknolojia bunifu zinazoleta mabadiliko ya haraka, Dira 2050 inaweka mikakati thabiti ya mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, yenye weledi, kipato cha kati ngazi ya juu, unaofikia thamani ya dola za Marekani trilioni moja, na wastani wa pato la mtu mmoja lenye thamani ya dola za Marekani 7,000 kwa mwaka.

Dira 2050 inalenga kuwa na jamii yenye mshikamano na utangamano ambayo watu wake wanaishi kwa haki, amani na kuheshimiana. Dira hii pia inalenga kuwa na wananchi wenye maarifa na ujuzi unaohitajika katika karne ya 21, ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, wakijitegemea na kuboresha maisha yao.

Dira 2050 inaweka dhamira ya kujenga uhimilivu wa taifa, kama msingi wa kukabiliana na mabadiliko yanayotokea duniani, na kufanikisha maendeleo endelevu. Miji na miji midogo inayochipukia inakuwa kwa kasi ambayo haijawahi kushuhudiwa. Ukuaji huo unatoa fursa za kukuza uchumi na kuboresha hali ya maisha. Hata hivyo, ukuaji huu unahitaji mipango madhubuti, jumuishi na shirikishi, inayowiana kati ya maendeleo ya mijini na vijijini huku ikizingatia uhifadhi wa mazingira.

Dira hii imeweka msisitizo mahsusi wa kuimarisha haki za binadamu, usawa wa kijinsia, na kuwawezesha vijana pamoja na watu wenye ulemavu. Masuala haya

yanaakisi misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na ni nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya maendeleo jumuishi na endelevu. Aidha, Dira inaweka azma ya Tanzania kuendelea kuwa mshirika mwaminifu, mwenye mchango chanya katika majukwaa ya maendeleo ya kikanda na dunia kwa ujumla.

## 2.1. Misingi ya Dira

Dira 2050 inaongozwa na misingi ifuatayo:

### 1. Demokrasia, Haki na Uhuru

Kila mtu anafurahia uhuru, ulinzi wa maisha yake na haki zote za msingi zilizowekwa kikatiba, zinazosimamiwa na mahakama zilizo huru, zinazozingatia makundi yote ya jamii wakiwemo wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na wazee.

### 2. Utu

Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kuthaminiwa utu wake, kulindwa na kuhakikishiwa faragha yake.

### 3. Amani na Umoja

Kila mtu anadumisha amani, umoja na mshikamano kama msingi wa maendeleo, anathamini na kulinda Muungano wetu kama tunu ya taifa, ambapo watu wote wanaheshimiana, na kuchangia katika kufanikisha malengo ya pamoja ya kitaifa.

### 4. Utajiri na Rasilimali Asilia

Haki ya nchi kumiliki kikamilifu na kutumia utajiri na rasilimali zake kwa manufaa ya Taifa na ustawi wa wananchi wake.

### 5. Utamaduni na Maadili ya Taifa

Taifa linalohifadhi, kukuza na kulinda maadili na tamaduni chanya kwa lengo la kuimarisha umoja na utambulisho wa kitaifa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

## 2.2. Malengo na Shabaha

Dira 2050 inalenga kufikia malengo na shabaha zifuatazo:

**Lengo Na. 1: Uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani.**

**Shabaha**

1. Nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu, unaofikia thamani ya dola za Marekani trilioni moja, na wastani wa pato la mtu mmoja lenye thamani ya dola za Marekani 7,000 kwa mwaka.
2. Kutokomeza umaskini uliokithiri kwa makundi yote.
3. Kuwa mzalishaji mkuu wa chakula barani Afrika na miongoni mwa nchi kumi bora duniani.

**Lengo Na. 2: Maisha bora na ustawi kwa wote.**

**Shabaha**

1. Mtanzania anaishi kwa wastani wa miaka 75, akifurahia maisha bora na afya njema.
2. Watoto wote wa kike na wa kiume wanapata malezi na makuzi bora ya utotoni,huku angalau asilimia 90 ya watoto wote wanafikia hatua stahiki za ukuaji ifikapo umri wa miaka mitano.
3. Kutokomeza vifo vya wajawazito, watoto wachanga na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.
4. Huduma bora za afya kwa wote.
5. Mfumo bora na jumuishi wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.
6. Watoto wote wa kike na wa kiume wana fursa sawa za kupata elimu ya awali yenye kujenga msingi imara kwa ajili ya kujifunza na kujielimisha bila ukomo.
7. Watanzania wote wanapata elimumsingi bora na angalau asilimia 25 wanapata elimu ya juu.
8. Upatikanaji wa huduma jumuishi za hifadhi ya jamii kwa wote.
9. Upatikanaji sawia wa maji safi na salama, huduma za usafi wa mazingira na nishati safi.
10. Angalau asilimia 50 ya Watanzania wana ajira zenye staha katika sekta rasmi.

11. Kuongezeka kwa matumizi ya nishati ya umeme kufikia wastani kwa mwaka wa 3,000 Kwh kwa kila mtu.

12. Tanzania kuwa kinara barani Afrika na miongoni mwa nchi kumi bora duniani katika kupunguza pengo la kijinsia kwa angalau asilimia 85.

**Lengo Na. 3: Taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija, na linalostahimili mabadiliko ya tabianchi.**

**Shabaha**

1. Kuwa na viwango vya juu vya uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na kuifanya Tanzania kuwa kati ya nchi kumi bora barani Afrika.

**Lengo Na. 4: Jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijitali katika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wake kimataifa.**

**Shabaha**

1. Jamii yenye umahiri wa kidijitali, ambapo angalau asilimia 70 ya wananchi wanatumia TEHAMA.

2. Zaidi ya asilimia 80 ya huduma za serikali zinapatikana kupitia mifumo ya kidijitali salama na jumuishi.

## 2.3. Muundo wa Dira

Dira 2050 imejengwa juu ya msingi wa utawala bora, amani, usalama na utulivu, unaotokana na mfumo imara wa kikatiba, utawala wa sheria na haki za binadamu. Tanzania imejizatiti kuboresha taasisi za kidemokrasia, kupambana na rushwa na kuhakikisha kunakuwa na uadilifu na uwajibikaji katika nyanja zote, zikiwemo sekta za umma na binafsi. Lengo ni kujenga utulivu unaohitajika katika kuvutia uwekezaji na kupata maendeleo ya muda mrefu.

Dira ina nguzo kuu tatu - Uchumi Imara, Jumuishi, na Shindani; Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii; na Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi. Nguzo hizi zinatoa mwelekeo na nyenzo muhimu kwa utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo ya Tanzania kuelekea mwaka 2050.

Nguzo ya kwanza, **Uchumi Imara, Jumuishi, na Shindani** inalenga kuifanya Tanzania kuwa kinara wa uchumi katika Afrika mashariki na bara la Afrika kwa ujumla. Lengo hili litafikiwa endapo kutakuwa na utulivu wa uchumi jumla, uendelevu wa sera za kifedha, kubuni vyanzo mbadala vya mapato na kuweka mazingira ya uwekezaji yanayotabirika. Hatua nyingine ni kukuza wajasiriamali wa ndani, kuboresha mazingira ya biashara, kuimarisha uwezo wa wadau wa sekta ya biashara na kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Nguzo ya pili, **Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii**, inajikita katika kujenga jamii yenye afya, elimu bora na mshikamano. Vipaumbele vya nguzo hii ni elimu bora inayolingana na mahitaji ya kijamii na kiuchumi kwa wakati uliopo. Msisitizo wa pekee unahitajika kwenye masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati. Muhimu pia ni huduma bora za afya kwa wote, upatikanaji wa maji safi na salama na usafi wa mazingira na nishati. Ujenzi wa jamii jumuishi, hususan kwa makundi yaliyoachwa nyuma, kukuza maadili na kuimarisha umoja wa kitaifa ni sehemu muhimu ya nguzo hii.

Nguzo ya tatu, **Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi,** inalenga kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya maliasili za taifa. Nguzo hii inalenga pia kudhibiti uharibifu wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuhifadhi bioanuai, ardhioevu na vyanzo vya maji, kudhibiti uchafuzi wa mazingira, usimamizi bora wa ardhi na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Nguzo hii inakwenda sambamba na Malengo Endelevu ya Dunia na hivyo kuimarisha uongozi wa Tanzania katika kutetea uhifadhi wa mazingira.

Dira 2050 inabainisha maeneo matano ambayo ni vichocheo vya kuharakisha utekelezaji wake. Vichocheo hivyo ni usafirishaji fungamanishi, sayansi na teknolojia, utafiti na maendeleo, mabadiliko ya kidijitali na nishati.

- **Usafirishaji Fungamanishi** utaifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara kikanda. Lengo hili litafanikiwa kwa kuboresha na kuunganisha miundombinu kama reli, bandari, anga na barabara ili kuongeza ufanisi katika usafirishaji wa bidhaa, huduma na watu, sambamba na kuimarisha mifumo ya kisheria na kodi na kuongeza weledi katika utoaji wa huduma.


- Upatikanaji wa **Nishati** ya uhakika utachochea ustawi wa jamii na maendeleo ya kiuchumi kwa kutoa suluhisho la kuaminika na nafuu ili kuchochea ukuaji wa viwanda, na kuongeza tija.

- Matumizi ya **Sayansi na Teknolojia** yatasaidia kuongeza ufanisi na tija katika uzalishaji na kuchochea mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Hili litafanikiwa kwa kuwekeza kwenye uvumbuzi, hasa kwenye sekta muhimu kama vile kilimo, afya na viwanda.

- **Utafiti na Maendeleo** utachochea uvumbuzi na upatikanaji wa taarifa muhimu kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi na kwa maendeleo ya kisekta. Kipaumbele kitawekwa kwenye ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu, vituo vya utafiti, sekta ya viwanda, kilimo na uzalishaji, ili kuongeza tija na maendeleo endelevu.

- **Mageuzi ya Kidijitali** yatachochea matumizi ya teknolojia ili kuboresha utoaji wa huduma, kuimarisha utawala bora, na ukuaji wa uchumi, huku yakipanua wigo wa ushiriki wa wananchi katika shughuli za kimaendeleo.

Kwa ujumla, Dira 2050 inatambua umuhimu wa sekta zenye uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko kufikia malengo ya kiuchumi na kijamii. Sekta hizo zitapewa kipaumbele ili kukuza ajira, kuongeza mauzo ya nje na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine, pamoja na kuchangia katika masoko ya ndani na nje. Baadhi ya sekta zenye fursa za kuleta mageuzi kuelekea 2050 ni kilimo, utalii, viwanda, ujenzi na mali isiyohamishika, madini, uchumi wa buluu, michezo na ubunifu, huduma za kifedha na sekta ya huduma. Mchoro ufuatao ni muhtasari wa muundo wa Dira 2050.




Muundo wa Dira 2050

# 3. MSINGI MKUU WA DIRA

## *Utawala, Amani, Usalama na Utulivu*

Dira 2050 imejengwa juu ya msingi mkuu wa utawala bora, amani, usalama na utulivu. Msingi huu unajumuisha hatua muhimu za kuheshimu Katiba, utawala wa kidemokrasia, mgawanyo wa madaraka na utamaduni wa kisiasa unaokuza ushirikishwaji na umoja wa kitaifa. Dira 2050 inasisitiza utawala wa sheria, ulinzi wa haki na uhuru wa msingi, usalama wa watu, pamoja na uimara wa asasi za kiraia. Masuala yenye umuhimu wa kipekee ndani ya Dira hii ni utumishi wa umma wenye weledi, uhuru wa taasisi mbalimbali, usawa wa kijinsia, umoja wa kitaifa na usalama wa taifa na mipaka ya nchi. Msingi mkuu hausimami pekee yake bali uko mtambuka, unatoshelezana na nguzo, vichocheo na sekta za kimageuzi.

Utawala wa sheria ambao ni kipengele muhimu cha utawala bora unakusudia kujenga jamii yenye usawa, uwajibikaji, haki na kuaminiana. Vilevile, unalenga kuhakikisha kwamba kunakuwa na uadilifu katika taasisi mbalimbali na uhuru na haki za msingi za jamii zinalindwa. Lengo jingine ni kuhakikisha kwamba rasilimali na huduma ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya watu zinapatikana kwa usawa. Vilevile, utawala bora unalenga kuweka mazingira muafaka ya kuimarisha utulivu na uwajibikaji ili kuwa na uchumi imara, jumuishi na shindani. Pamoja na vipengele hivi, kuna umuhimu mkubwa wa kupambana na rushwa. Hivyo, masuala ya kipaumbele katika ajenda hii ni kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, kujenga taasisi imara, kuweka mifumo madhubuti ya kisheria na kusimamia uwazi na uwajibikaji.

Msingi mkuu wa Dira unasisitiza umuhimu wa jamii kuwa jumuishi na shirikishi, yenye amani na utulivu. Jamii tulivu hujengwa kupitia familia imara, jamii zenye mshikamano na utambulisho wa pamoja wa kitaifa. Jitihada za awali kabla na baada ya uhuru, za kuondoa tofauti za kikabila na kidini, zilistawisha umoja wa kitaifa, huku lugha ya Kiswahili ikiwa nyenzo madhubuti ya kuunganisha jamii. Hatua hizi zilikuza utamaduni wa kisiasa uliojenga misingi imara ya amani na utulivu, ambayo ni muhimu katika kutekeleza ajenda ya maendeleo.

Kwa ujumla, msingi mkuu wa Dira 2050 unahakikisha kwamba maeneo yote ya Dira yanafungamana ili kuleta ufanisi. Dira inakusudia kuimarisha utawala bora, haki za binadamu, demokrasia na uwajibikaji, sambamba na juhudi za kukuza uwazi katika matumizi ya rasilimali za umma na kuendeleza uadilifu katika ngazi zote za utendaji. Kwa kuimarisha mifumo ya utawala bora, kuendeleza ushiriki jumuishi wa wananchi, na kulinda amani, Tanzania inaweka msingi imara wa kuelekea kwenye taifa lenye uthabiti, ustawi na usawa kwa wote.

## 3.1 Maeneo ya Kipaumbele

### 3.1.1 Utawala Bora na Haki

Utawala bora ni mhimili wa taifa imara, jumuishi, na lenye ustawi. Unahakikisha kwamba kunakuwa na usimamizi wa wazi wa rasilimali za umma sambamba na kuweka mazingira yanayowawezesha wananchi kustawi kijamii, kiuchumi, kisiasa, na kiutamaduni. Jamii inayothamini utawala bora inaweka umuhimu kwenye uwajibikaji, mapambano dhidi ya rushwa, ulinzi wa haki za msingi za raia, na kuhakikisha fursa sawa kwa wote bila kujali tofauti za kijinsia, kiuchumi, kijamii au hali ya ulemavu. Katika muktadha huu, vyombo vya habari huru na vinavyojitegemea ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha utawala bora na uwajibikaji. Kadhalika, asasi za kiraia zina mchango muhimu katika kukuza demokrasia, kulinda haki za binadamu na kuchangia jitihada za kuboresha huduma za jamii.

Haki ina uhusiano wa karibu na utawala bora, hasa kwa kuzingatia mgawanyo sawa wa rasilimali na fursa mbalimbali za maendeleo. Haki inalinda maslahi ya wanajamii ambao wako katika mazingira tete, inakuza usawa na kuhakikisha utu na usalama wa kila mwananchi unalindwa. Ili kutimiza lengo la upatikanaji haki, yatahitajika mabadiliko makubwa, utashi wa kisiasa, na jamii yenye maarifa na dhamira ya kuwawajibisha viongozi wao. Utawala bora na haki pamoja zinaunda mazingira muafaka ya usawa na ustawi wa jamii.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuboresha demokrasia na utawala bora. Mageuzi muhimu yaliyofanyika ni pamoja na kuimarisha uhuru wa mahakama, kukuza mfumo wa vyama vingi na kuwepo kwa chaguzi zilizo wazi, huru na kufanyika kwa vipindi vinavyofahamika. Mageuzi haya yameongeza uwazi wa kisiasa na uwajibikaji. Vilevile, juhudi zimefanyika kupambana na rushwa katika ngazi mbalimbali za utawala na kuboresha haki za binadamu. Maendeleo haya yameimarisha utulivu wa kisiasa na kuongeza imani ya wananchi kwa serikali.

Licha ya mafanikio haya, Tanzania bado inakabiliwa na changamoto kadhaa za kiutawala. Kwa mfano, vyombo vinavyohusika na utoaji wa haki bado vinakabiliwa na changamoto za kiutendaji zinazozuia kufikiwa kwa viwango vya juu vya ufanisi katika kuwahudumia wananchi ipasavyo. Matumizi mabaya ya madaraka ya baadhi ya viongozi wa umma wanaokwenda kinyume na kuvuka mipaka yao ya kisheria yamekuwa mengi na ya kawaida.

Aidha, ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika ngazi za maamuzi bado ni mdogo. Ukatili wa kijinsia na dhidi ya watoto umeenea kwingi, hata kwenye siasa. Japokuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua za kukabiliana na rushwa katika sekta mbalimbali, hususan sekta ya umma, changamoto hii bado ipo na inaathiri kwa kiasi kikubwa juhudi za kukuza haki za kijamii na kufanikisha maendeleo jumuishi. Changamoto hizi zinadhihirisha haja ya kuwa na mageuzi ya kina ili kuimarisha taasisi na mifumo ya kutoa huduma kwa nia ya kuleta maendeleo endelevu.

*Matarajio*

a) Taifa la kidemokrasia linalozingatia utawala wa sheria, haki za binadamu na upatikanaji wa haki jamii.

b) Utawala unaozingatia uadilifu na unaoongoza mapambano dhidi ya rushwa kama msingi wa uwajibikaji, uwazi na haki.

c) Taasisi imara zinazofuata misingi ya usawa na haki, zinazotoa huduma kwa ufanisi bila upendeleo ili kujenga imani ya wananchi.

d) Uongozi wenye maono, unaowajibika na wenye kushirikisha jamii, hususan vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

e) Mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria unaoakisi muafaka wa kitaifa, ili kuhakikisha kuwepo kwa haki na usawa.

f) Sekta ya habari inayofanya kazi kwa uhuru, uwazi na inayochochea uwajibikaji, uhuru wa kujieleza na upatikanaji sawa wa taarifa kama mhimili wa demokrasia hai.

g) Asasi za kiraia zenye uwezo na ufanisi, zinazochangia kwa umakini katika kuimarisha demokrasia, kukuza na kuthamini sauti za wananchi, na kuhakikisha uwajibikaji kwa maslahi ya Taifa.

h) Jamii salama na isiyo na unyanyasaji wa kijinsia na watoto, ambapo kila mtu, ikiwemo watu wenye ulemavu na wazee, yuko salama, ana furaha, anaheshimiwa na kuwezeshwa.

### 3.1.2 Serikali za Mitaa Imara na Zenye Ufanisi

Serikali za mitaa zilizo bora na zenye nguvu ni nguzo muhimu katika kufikia malengo makuu ya Dira 2050 kwa kukuza ushirikishwaji, demokrasia na kuhakikisha kwamba sauti za jamii zinachangia katika kuchora ramani ya maendeleo ya taifa. Katika muktadha huu, serikali za mitaa zina umuhimu mkubwa kwani zinalenga kuhakikisha kuwa maamuzi, ukusanyaji na ugawaji wa rasilimali vinakwenda sambamba na mahitaji ya maeneo husika. Umuhimu wa serikali za mitaa unabainika zaidi katika kukuza umoja wa kitaifa, zinajenga daraja kati ya wananchi na serikali kuu. Vilevile, serikali za mitaa zina mchango mkubwa katika kuhakikisha kwamba sera za kitaifa na mahitaji ya jamii vinakwenda sambamba ili kuchochea maendeleo endelevu, jumuishi na yanayokabili changamoto zinazowakabili wananchi. Serikali za mitaa imara, zinakuza mapato, kuimarisha mifumo ya kodi, kukuza ushiriki wa jamii, kuboresha utoaji wa huduma na kuhimiza uwajibikaji. Hali hii itawezesha kuwepo kwa mfumo wa utawala unaokidhi mahitaji ya wananchi na kukuza umoja wa jamii na taifa.

Serikali za mitaa nchini Tanzania zimepitia mabadiliko mbalimbali kwa nyakati tofauti. Mnamo mwaka 1962, serikali ilifuta utawala wa kimila na kuanzisha serikali za mitaa, mamlaka za miji na halmashauri za wilaya. Mwaka 1972, mfumo wa serikali za mitaa nao ulifutwa na kuanzishwa kwa ugatuzi wa madaraka ambapo ofisi za mikoa na wilaya ziliwekwa chini ya udhibiti wa serikali kuu. Hata hivyo, kukosekana kwa ushiriki wa wananchi kuliathiri utoaji wa maamuzi sahihi, na hivyo kushinikiza urejeshwaji tena wa mamlaka za miji mwaka 1978, na serikali za mitaa mwaka 1982 ili kuimarisha ushiriki wa wananchi na utoaji wa huduma. Mabadiliko mengine makubwa yalifanywa mwaka 1996 ili kuimarisha ushiriki wa wananchi, uwajibikaji na kuongeza makusanyo ya fedha.

Licha ya juhudi hizi, mfumo wa serikali za mitaa nchini Tanzania umekuwa na changamoto ya kukosekana sera zinazotabirika na hivyo kuathiri uendelevu wa taasisi hizo. Vilevile, serikali za mitaa zilikosa uhuru wa kufanya maamuzi, sambamba na kukabiliwa na uhaba wa watumishi, uwezo mdogo wa watendaji, utegemezi wa kifedha na vitendo vya rushwa. Hali iliyoathiri utawala bora na utoaji wa huduma kwa wananchi.

***Matarajio***

a) Mamlaka za serikali za mitaa jumuishi, zinazojitegemea, zinazowajibika kwa wananchi na kuendeshwa bila rushwa.

b) Ushirikiano wa wazi na wenye tija kati ya serikali kuu na serikali za mitaa, unaohakikisha mgawanyo endelevu wa rasilimali na utoaji wa huduma bora kwa ufanisi.

c) Serikali za mitaa zinazoimarisha mshikamano wa kijamii na kuweka mazingira wezeshi kwa biashara na uwekezaji.

d) Ukuaji jumuishi na mgawanyo sawia wa rasilimali ili kukuza ustawi, kuongeza mshikamano na kasi ya utatuzi wa changamoto za kijamii.

e) Mfumo wa utumishi katika serikali za mitaa uliojikita kwenye misingi ya uadilifu na unaozingatia sifa na uwezo katika kuajiri na upandishaji vyeo ili kuendeleza weledi na ufanisi katika utoaji wa huduma.

### 3.1.3 Utumishi wa Umma Unaowajibika

Utumishi wa umma bora na unaowajibika ni msingi muhimu wa utawala bora katika kusimamia utekelezaji wa sera mbalimbali, utoaji wa huduma na uratibu wa mipango ya kitaifa. Kwa kutambua mchango wa utumishi wa umma katika ujenzi wa Taifa, Tanzania inaendeleza maboresho ya kimfumo ambayo yanalenga kuimarisha ufanisi, weledi na uwajibikaji. Maboresho haya ni pamoja na mifumo ya kupima utendaji kazi, mafunzo ya kujenga uwezo wa watumishi na matumizi ya teknolojia za kidijitali ili kurahisisha michakato ya utendaji kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi.

Licha ya jitihada hizi, bado kuna mapungufu kadhaa yanayoikabili na kuiathiri sekta ya umma - uhaba wa wafanyakazi, ujuzi na uwezo mdogo katika utendaji. Desturi na utaratibu wa kuajiri watumishi wa umma bila ya kufuata misingi ya uwazi na weledi vinaathiri uwezo wa taasisi za umma katika kutoa huduma. Changamoto hizi zinakwamisha utekelezaji wa mipango ya Serikali na zinaweza kufifisha imani ya wananchi kwa Serikali.

Kuelekea mwaka 2050, utumishi wa umma unaowajibika, wenye weledi, uadilifu na unaozingatia misingi ya utawala bora utakuwa chachu ya maendeleo.

***Matarajio***

a) Utumishi wa umma unaofanya kazi kwa ufanisi, uwajibikaji, uadilifu, uwazi na wenye kupambana na rushwa ili kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa maendeleo na manufaa ya wote.

b) Utumishi wa umma unaozingatia viwango vya juu vya weledi, unaopatikana na kuendelezwa kwa kufuata misingi ya haki, umahiri na utendaji bora.

### 3.1.4 Amani, Usalama na Utulivu

Amani, usalama na utulivu ndiyo msingi utakaojenga taifa lenye mafanikio na umoja, litalokuza uchumi na kuwezesha mshikamano wa kijamii. Amani katika jamii inaanzia kwenye familia. Hii ni taasisi ya awali ambayo inapanda mbegu ya utamaduni wa amani na kustawisha maadili muhimu kama vile desturi, heshima, busara, utatuzi wa migogoro, na ushirikiano. Maadili haya yanapolelewa ndani ya familia, ndipo yanapoenea katika jamii pana na kuimarisha utangamano. Jamii zilizojengwa katika misingi hii zinakuwa na uwezo bora wa kusimamia migogoro kwa amani na kuzuia vurugu na machafuko. Aidha, familia imara ni msingi wa taifa lenye utulivu, usalama na amani.

Kwa muda mrefu Tanzania imekuwa ikithamini umuhimu wa amani, usalama na utulivu, kama njia ya kukuza umoja wa kitaifa na nguvu ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Tanzania imejizatiti kuimarisha utawala shirikishi wa ndani, kuheshimu haki za binadamu, na kuzingatia utawala wa sheria, na hivyo kuweka mazingira muafaka ya amani na maendeleo. Kikanda, Tanzania imekuwa mtetezi thabiti wa amani, ikichukua nafasi yake katika juhudi za upatanishi, misheni za kulinda amani, na kuhimiza mazungumzo ya amani na maridhiano katika ukanda wa Afrika Mashariki na Maziwa Makuu. Kimataifa, michango yake katika operesheni za kulinda amani inadhihirisha dhamira yake ya kukuza amani na utulivu duniani.

Hata hivyo, matishio dhidi ya amani, usalama na utulivu wa Tanzania bado yapo. Kukosekana kwa usawa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, migogoro ya ardhi, na ukosefu wa ajira kwa vijana vinaendelea kuwa tishio kwa usalama. Aidha, mivutano ya kijiopolitiki, mivutano ya kibiashara, na kuporomoka kwa mifumo ya

kimataifa iliyokuwa ikiheshimu sheria, inaweza kuwa na taathira kwenye hali ya jumla ya usalama wa nchi. Ili kulinda usalama na utulivu, Tanzania inahitaji kuwa macho, kuhakikisha miundombinu yake ya ulinzi ina nguvu, huku ikijihusisha kikamilifu katika diplomasia, kuzuia migogoro, kujenga amani, na kukuza jitihada za maridhiano ya kikanda na kimataifa.

***Matarajio***

a) Muungano imara na thabiti unaoendeleza umoja wa kitaifa, amani, utulivu, na ustawi wa pamoja kwa wananchi wote kuanzia ngazi ya familia.


b) Taifa lenye uwezo wa kubaini na kuchukua hatua mapema dhidi ya matishio ya usalama na maslahi ya taifa, huku likiimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kujenga ustahimilivu dhidi ya changamoto za ndani na za nje.

c) Taifa linalothamini na kulinda watu wake wote, wakiwemo watu wenye ulemavu, wazee na wanawake.

d) Taifa ambalo ni kielelezo cha amani na maelewano, likiwa na nafasi muhimu katika kuleta utulivu wa kikanda kupitia juhudi za ushirikiano na upatanishi, na kushiriki kikamilifu katika utatuzi wa migogoro.

# 4. NGUZO ZA DIRA

Dira 2050 inajengwa juu ya nguzo tatu, ambazo ni muhimu katika kufika lengo la Tanzania kuwa taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea. Nguzo ya kwanza inalenga kujenga *uchumi imara, jumuishi na wenye ushindani,* kwa kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji ili kuendeleza ukuaji endelevu. Nguzo ya pili inajikita katika kujenga *uwezo wa watu na maendeleo ya jamii*. Nguzo ya tatu inalenga *uhifadhi endelevu wa rasilimali za asili za Tanzania*, kwa kudhibiti uharibifu wa mazingira, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kuhifadhi bioanuai, ardhioevu na vyanzo vya maji. Nguzo hizi zinafanya kazi kwa kutegemeana, zikiimarishwa na vichocheo na msingi mkuu wa dira. Aidha, nguzo hizi zinasaidia sekta za mageuzi kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mfumo huu ni muhimu kwa kufanikisha maendeleo ya kijamii, kiuchumi, uhifadhi wa mazingira na ushirikishaji wa kijamii. Sehemu zinazofuata zinaelezea kila nguzo kwa kina.



## 4.1. Nguzo ya Kwanza: Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

Uchumi imara, jumuishi na shindani ni moja ya nguzo kuu ya kujenga taifa lenye ustawi, kwani nguzo hii inafungua fursa za kiuchumi na hivyo kuweka mazingira ya kupunguza umaskini na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wote. Uchumi imara utahakikisha kwamba maendeleo ya kiuchumi yanakuwa na taathira chanya kwa jamii na kuwanufaisha wananchi wote. Katika muktadha huu, Tanzania imeendelea kupiga hatua za kiuchumi, ambapo uchumi umeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.2 kwa mwaka katika kipindi cha miongo miwili iliyopita.

Hata hivyo, ukuaji huu ambao umechangia utulivu wa uchumi-jumla, bado uko katika kiwango cha chini, ikilinganishwa na rasilimali za nchi, na maoteo ya kukua kwa asilimia 8, kama ilivyobashiriwa katika Dira 2025. Kutokana na hilo, uchumi haukuweza kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa. Badala yake, uchumi ulikosa sekta mseto za kuchochea ukuaji, uzalishaji ulikuwa mdogo, wigo wa masoko ulikuwa finyu na mauzo ya nje yalipungua. Hali hii iliathiri uzalishaji wa ajira, upatikanaji wa fedha za kigeni na kudhoofisha uhimilivu wa uchumi dhidi ya mitikisiko ya ndani na nje.  Aidha, wananchi wengi, hususani wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, wameendelea kubaki katika sekta isiyo rasmi.

Ili kufanikisha malengo ya Dira 2050, ni lazima kujenga uchumi mseto, shirikishi, na shindani wa kimataifa. Uchumi huu utategemea rasilimali za ndani na kuendeshwa kwa misingi ya sera madhubuti na mifumo bora ya udhibiti inayochochea ukuaji wa biashara na ujasiriamali, kurasimisha sekta isiyo rasmi, na kuvutia uwekezaji mkubwa wa ndani na nje ya nchi.

### Maeneo ya Kipaumbele

#### 4.1.1 Uchumi-jumla Tulivu na Unaotabirika

Utulivu na kutabirika kwa uchumi ni muhimu kwa kukuza uchumi imara na endelevu. Utulivu wa uchumi hupatikana pale ambapo viashiria muhimu vya kiuchumi vinakua katika uwiano mzuri, hususan mahitaji na uzalishaji wa ndani, mapato na matumizi ya serikali, pamoja na akiba na uwekezaji. Tanzania imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei na viwango vya ubadilishaji wa fedha kwa ufanisi. Mfumuko wa bei umeendelea kubaki kwenye tarakimu moja kwa takriban muongo mmoja, huku thamani ya sarafu ikiendelea kuimarika.

Kutabirika kwa uchumi  kunapimwa kwa viashiria mbalimbali vinavyoakisi sera wezeshi za uchumi, sheria, kanuni za udhibiti, pamoja na mifumo ya usimamizi wa fedha na kodi. Hata hivyo, mabadiliko ya mara kwa mara ya sera za ndani na miundo ya taasisi yalichangia ukosefu wa utulivu katika miongozo ya serikali na kudhoofisha utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo. Hali hiyo inaweza kusababisha kutokuaminika kwa viashiria vya uchumi kwa ajili ya maamuzi ya biashara na uwekezaji. Kwa mantiki hiyo, kuna umuhimu wa kuwa na  mfumo madhubuti wa uchumi unaotabirika, sambamba na mgawanyo wa wazi wa

majukumu kati ya Serikali, kama kiongozi wa mabadiliko na sekta binafsi, kama kichocheo cha mabadiliko.

***Matarajio***

a) Mazingira tulivu ya kiuchumi yanayozingatia uwiano kati ya uzalishaji na mahitaji ya ndani, urari wa malipo, mapato na matumizi ya serikali pamoja na viwango vya akiba na uwekezaji.

b) Sera za uchumi zinazotabirika na kuzingatia uwazi, pamoja na mfumo thabiti wa kisheria, sera za kifedha na kodi, ili kuvutia uwekezaji endelevu wa ndani na nje.

### 4.1.2 Mfumo Endelevu wa Kibajeti

Mfumo endelevu wa fedha unahusisha uwezo wa serikali kuendana na sera zake za matumizi, kodi na madeni kwa muda mrefu bila kuyumba. Mfumo huu ni msingi wa uchumi imara na shindani. Katika kipindi cha miongo miwili na nusu iliyopita, Tanzania imeendelea kuimarisha uwezo wake wa kifedha na kuboresha usimamizi wa matumizi kupitia mabadiliko kadhaa. Maboresho hayo ni pamoja na kupanua wigo wa kodi, kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kutumia teknolojia za kidijitali, kuongeza uwazi katika utoaji wa huduma na kutoa elimu kwa walipa kodi. Pia yanajumuisha uboreshaji wa mipango na bajeti, usimamizi wa matumizi na michakato ya ukaguzi. Pamoja na jitihada hizi, wigo wa kodi bado ni finyu, ukitegemea vyanzo vichache vya mapato. Aidha, uwiano kati ya makusanyo ya kodi na pato la taifa ni asilimia 11.9 kwa mwaka 2022/23, ambayo ni ndogo ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.1 wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Vilevile, sera za mapato kwa kiasi kikubwa zimejikita katika kukuza mapato kwa kuongeza viwango vya kodi kwa walipa kodi waliopo, badala ya kuwezesha ukuaji wa biashara ili kupanua wigo wa walipa kodi. Hali hii, pamoja na usimamizi duni wa kodi, imesababisha kuzorota kwa mahusiano kati ya walipa kodi na mamlaka za ukusanyaji kodi.

Ukuaji wa matumizi ya Serikali umeongeza mahitaji ya mikopo na hivyo, kupunguza ukwasi wa sekta binafsi katika soko la fedha. Ingawa usimamizi wa matumizi ya Serikali umeimarika katika suala la uangalizi, bado haujaweka kipaumbele kwenye matumizi ya kimkakati na ufanisi.

Usimamizi wa deni la taifa pia ni muhimu katika kuhakikisha uwiano mzuri wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali unaotokana na mikakati madhubuti ya uwekezaji wa umma. Pamoja na kwamba deni la taifa limeendelea kuwa himilivu, kama inavyothibitishwa na taasisi za kimataifa za tathmini ya madeni, juhudi za dhati zinahitajika katika kuimarisha uwezo wa kifedha na uimara wa uchumi.

***Matarajio***

a) Mfumo wa kodi wa haki na wenye ufanisi unaochochea ukuaji endelevu na ustawi wa muda mrefu kwa kuongeza uwiano kati ya kodi na pato la Taifa, huku ukichangia maendeleo endelevu.

b) Mfumo wa kodi unaotabirika na wa uwazi, unaohamasisha utii wa sheria na kurahisisha uanzishaji, usajili na ukuaji wa biashara ili kuongeza ajira na kuchochea ukuaji wa uchumi.

c) Usimamizi madhubuti wa deni la taifa unaohakikisha uhimilivu na mgawanyo bora wa rasilimali katika maeneo ya kipaumbele ya maendeleo.

d) Matumizi ya fedha za umma yanayozingatia vipaumbele, thamani ya fedha na matokeo makubwa kiuchumi.

e) Uwiano mzuri wa matumizi ya Serikali baina ya uwekezaji wa miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

### 4.1.3 Vyanzo Anuai na Bunifu vya Mapato

Uwezo wa kugharamia shughuli za maendeleo nchini unategemea ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, mikopo ya ndani na nje, uwekezaji kutoka nje, na misaada rasmi ya maendeleo. Ingawa vyanzo hivi bado vinahitajika, ubunifu katika kutafuta vyanzo vipya vya mapato ni muhimu ili kupanua wigo wa mapato na kuongeza uwezo wa kugharamia shughuli za maendeleo. Miongoni mwa fursa zinazoweza kutumika ni ushirikiano wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, masoko ya mitaji, misaada ya hiari, uwekezaji wa hisa binafsi, na mitaji ya ubia. Katika juhudi za kuongeza vyanzo vya mapato, Tanzania imetekeleza mipango mbalimbali ikiwemo kuanzishwa kwa soko la mitaji na mifumo wezeshi, kama vile Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Hati Fungani na Soko la Hisa la Dar es Salaam. Aidha, Serikali imeunda mifumo ya kitaasisi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ili kukuza ushirikiano kati ya sekta hizo.

Benki Kuu ya Tanzania imechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya masoko ya fedha kwa kuimarisha mazingira wezeshi ya ukuaji wa masoko hayo. Hatua hizi zinajumuisha kuweka miundombinu thabiti ya masoko ya fedha, kutunga sheria muafaka na kuwezesha matumizi bunifu ya nyaraka za kifedha katika masoko ya fedha na mitaji. Moja ya mafanikio makubwa ya juhudi hizi ni ongezeko kubwa la miamala ya fedha kwa njia ya simu. Vilevile, Serikali imeweka mazingira wezeshi ya kikodi ili kuvutia uwekezaji katika masoko ya fedha, ikiwa ni pamoja na kupunguza kodi ya makampuni, kuondoa kodi kwenye gharama za uorodheshaji wa awali wa hisa, pamoja na kufuta ushuru wa stempu na kodi ya faida ya mtaji kwenye biashara ya uwekezaji wa hisa.

Pamoja na jitihada hizi, bado kuna uelewa mdogo kuhusu dhana ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi. Vilevile, masoko ya mitaji na fedha bado hayajafikia viwango vya kuridhisha. Soko la fedha limejikita katika uwekezaji wa dhamana za serikali, ambazo hutoa faida kubwa bila ya hasara. Hali hii inasababisha sekta muhimu kama vile kilimo, biashara ndogo na za kati, nishati na utalii kukabiliwa na changamoto ya kupata mitaji katika soko la fedha.

Kwa kuendelea na mageuzi haya na kuandaa mikakati mipya, Tanzania ina nafasi ya kuimarisha mfumo wake wa upatikanaji wa mitaji ili kukidhi mahitaji ya uchumi unaokua na kuhakikisha ustawi wa muda mrefu. Hatua hiyo inajumuisha kuendeleza masoko ya fedha na mitaji, pamoja na kukuza uelewa na kuhamasisha utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, ili kuwezesha ukuaji endelevu na ongezeko la uwekezaji.

***Matarajio***

a) Taifa linalotumia kwa ufanisi ushirikiano wa ubia kati ya sekta za umma na binafsi ili kuleta mabadiliko na kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

b) Soko la fedha linaloongozwa kwa uwazi na ufanisi kwa kuzingatia kanuni na taratibu zinazofanikisha shughuli zake bila upotoshaji na linalotoa fursa sawia za upatikanaji wa rasilimali.

c) Soko madhubuti la mitaji linalofanya kazi kwa uwazi, lenye vyanzo bunifu na mbadala vya fedha, ili kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi, za kuaminika na za ubora wa hali ya juu kwa wadau wote.

d) Ubunifu na uvumbuzi unaochochea ukuaji na ustahimilivu wa sekta za uzalishaji ili kuziwezesha kupata mikopo ya kibiashara na kujiendesha kwa ufanisi.

e) Mfumo jumuishi wa kifedha unaoongozwa na sera na mikakati ya uwezeshaji wa wananchi wote, huku ukiweka mkazo maalum kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

f) Jamii inayothamini ujasiriamali na yenye wajasiriamali wenye uthubutu na usimamizi bora wa biashara kwa ukuaji endelevu na urithi wa mali kwa vizazi vijavyo.

g) Mfumo thabiti wa kusaidia kampuni zinazochipukia ambao unaziunganisha na taasisi za mitaji na uwekezaji ili kuongeza uwezo wao katika ubunifu, biashara na matumizi bora ya teknolojia za kidijitali.

### 4.1.4 Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji

Uchumi imara na endelevu unategemea kuwepo kwa mazingira mazuri ya kufanya biashara. Mnamo mwaka 2018, Tanzania ilizindua Mpango Mkakati wa Mageuzi ya Sheria ya Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini. Mpango huu ulilenga kuimarisha ufanisi katika mifumo ya kisheria, kurahisisha mchakato wa usajili na usimamizi wa biashara na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Vipaumbele vikuu vilikuwa ni kupitia upya sheria na kanuni, kupunguza kodi na ada zisizo na ufanisi, na kuboresha uwezo wa taasisi za udhibiti ili kuzifanya zijielekeze zaidi katika kuchangia ukuaji wa sekta ya biashara badala ya kuweka mkazo katika makusanyo ya mapato pekee.

Pamoja na juhudi hizo, changamoto mbalimbali zimeendelea kuyagubika mazingira ya biashara nchini, ikiwemo gharama na muda mkubwa wa usajili na ukosefu wa mitaji. Kikwazo kingine ni urasimu katika utendaji, jambo linaloongeza muda ambao wawekezaji wanachukua kukamilisha taratibu za awali za kuidhinisha biashara na uwekezaji. Aidha, uendeshaji wa biashara umeendelea kuwa na udhibiti uliokithiri, ukiathiri utaratibu wa kodi na mapato kwa bidhaa zenye thamani kubwa, migongano ya sera, sheria na kanuni, na kuwepo kwa muingiliano wa majukumu ya taasisi za udhibiti. Suala hili limezifanya biashara kubeba mzigo mkubwa wa kodi, ada na ongezeko la gharama kutokana na masharti mengi ya leseni, vyeti na vibali.

Ili kushughulikia changamoto hizi, ni lazima kujenga mazingira wezeshi ya kibiashara yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuvutia uwekezaji. Mageuzi haya yanapaswa kurahisisha taratibu, kupunguza vikwazo vya kisheria, kuondoa tozo zisizo na tija na kufungamanisha sera na taasisi ili kuimarisha mazingira ya biashara yenye ushindani na ufanisi.

Kwa ujumla, mapinduzi makubwa yanahitajika katika kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, hususan katika kubadili sekta ya umma kutoka kuwa mdhibiti, kwenda kuwa mwezeshaji wa biashara na uwekezaji.

***Matarajio***

a) Kuwa moja kati ya nchi tatu zinazoongoza Afrika kwa kuvutia uwekezaji na urahisi wa kufanya biashara.

b) Kuwa na sera, sheria na kanuni wezeshi zinazopunguza udhibiti uliokithiri na zinazochochea ukuaji wa biashara za ndani pamoja na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje.

c) Kuwa na mfumo imara wa kidijitali, unaoendeleza biashara zinazochipukia kupitia sera, ufadhili, mitaji na sheria zinazoharakisha ukuaji ili kuongeza ajira na kuimarisha uchumi.

d) Kuwa na jamii yenye utamaduni wa kuweka akiba na uwekezaji kwa ajili ya kuendeleza biashara, kuongeza kipato na kuimarisha hali ya maisha.

e) Kuwa na sekta ya umma iliyoandaliwa kuwezesha na kufanikisha biashara na uwekezaji.

### 4.1.5 Sekta Binafsi Imara

Sekta binafsi ni muhimu katika kukuza uchumi imara, jumuishi na shindani. Kuwepo kwa biashara ndogo, za kati na kubwa zinazomilikiwa na wafanyabiashara wa ndani na wa kigeni, pamoja na mashirika ya umma ya kibiashara, kunaimarisha ushiriki wa nchi katika soko la kimataifa, kuchochea ubunifu, utulivu na ustahimilivu wa kiuchumi na kuhakikisha ukuaji endelevu wa biashara unaoendana na mabadiliko ya soko.

Katika kuimarisha sekta ya biashara nchini, mashirika ya kibiashara ya umma yamekuwa na mchango mkubwa, yakichochea ajira na ukuaji uchumi kupitia uwekezaji katika sekta za kimkakati kama vile nishati, usafirishaji, miundombinu na uzalishaji. Hata hivyo, kutokana na utendaji hafifu, uwezo mdogo wa uzalishaji na usimamizi dhaifu, mashirika mengi yameshindwa kujiendesha na kuleta manufaa yaliyotarajiwa. Katika kukabiliana na hali hii, katikati ya miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990, Tanzania ilifanya mabadiliko makubwa, ikilenga kubinafsisha mashirika haya, ikiwa ni sehemu ya mpango wa kuelekea kwenye uchumi wa soko.

Hata hivyo, mabadiliko haya hayakuweza kuyajengea uwezo mashirika ya umma ya kibiashara ili kuwa shindani katika soko huria. Mashirika haya yaliendelea kutegemea ruzuku kutoka Serikalini, hali iliyoyapa kinga dhidi ya ushindani wa moja kwa moja na kampuni binafsi. Hali hii imesababisha kudorora kwa uchumi na kupungua kwa ufanisi wa sekta binafsi katika kuchangia maendeleo ya taifa. Ili kujenga sekta imara ya biashara, kunahitajika mageuzi ya kisera, kiutawala na kiutendaji. Mageuzi haya yanapaswa kubainisha kwa uwazi maeneo ya kimkakati ya uwekezaji kwa mashirika ya umma ya kibiashara, sambamba na kufungua milango kwa sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika maeneo mengine ya uchumi wa taifa kwa tija.

Kwa upande mwingine, sekta binafsi nchini inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazozuia uwezo wake wa kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya taifa. Mojawapo ni umiliki wa sehemu kubwa ya sekta hiyo kudhibitiwa na kundi dogo la watu. Kwa muktadha huo, uwezo wa sekta binafsi kuchangia kwa ufanisi katika maendeleo ya taifa unakuwa mdogo. Changamoto nyingine ni kuwepo kwa mazingira ya kisheria yaliyogubikwa na utaratibu mgumu, ikiwa ni pamoja na mchakato wa usajili, mabadiliko sera yasiyotabirika na mwingiliano wa taasisi za udhibiti, vimekuwa kikwazo kikubwa kwa ukuaji wa sekta binafsi nchini.

Changamoto hizi zinaongeza gharama za uendeshaji wa biashara na kufifisha jitihada za kuvutia uwekezaji wa ndani na wa kigeni. Aidha, licha ya kuwepo kwa sera zinazolenga kuwawezesha wawekezaji wazawa, utekelezaji wake bado ni hafifu, hivyo kupunguza mchango wao katika sekta binafsi.

Aidha, sekta binafsi inakumbana na vikwazo katika upatikanaji wa mitaji, ikiwemo viwango vya juu vya riba, masharti magumu ya dhamana, na kutokuwepo kwa masoko ya mitaji yanayokidhi mahitaji, ambayo yanaathiri zaidi ukuaji wa biashara ndogo na za kati. Ukosefu wa miundombinu unazidisha changamoto hizi, ambapo mtandao duni wa usafiri, umeme usio wa uhakika, na matumizi madogo ya fursa za kidijitali vinakwamisha uzalishaji na ushindani. Aidha, ujuzi usiokidhi viwango kutokana na kutokuwepo kwa uwiano kati ya maarifa ya wahitimu na mahitaji halisi ya soko la ajira umesababisha pengo kubwa la nguvukazi yenye stadi stahiki zinazohitajika katika kuendesha uchumi wa kisasa. Wakati huo huo, utitiri wa kodi, usimamizi wa kodi usioridhisha, na kukua kwa sekta isiyo rasmi huathiri maendeleo ya sekta rasmi. Kukabiliana na changamoto hizi kwa pamoja ni hatua muhimu ya kufungua uwezo mkubwa wa sekta binafsi kuwa injini ya mabadiliko ya kweli ya kiuchumi nchini.

***Matarajio***

a) Mfumo wa uwekezaji unaobainisha maeneo ya uwekezaji kati ya mashirika ya umma ya kibiashara na sekta binafsi ili kuharakisha ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu.

b) Utumishi wa umma unaotambua umuhimu wa maendeleo ya sekta binafsi kwa kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji.

c) Sekta binafsi shindani, thabiti, jumuishi na inayowajibika, inayochangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

d) Mashirika ya umma ya kibiashara yanayoendeshwa kwa uwazi na ushindani, yanayojitegemea na yenye kuleta faida, na yanayovutia uwekezaji huku yakishirikiana kikamilifu na sekta binafsi ili kukuza uchumi.

e) Sekta ya wajasiriamali wadogo na wa kati iliyoimarika, ya kisasa na iliyorasimishwa, ikifanya kazi sambamba na makampuni bunifu na shindani kimataifa, katika kuendeleza ukuaji wa uchumi na ustawi wa kijamii wa taifa.

### 4.1.6 Ushirikiano wa Kimkakati Kikanda na Kimataifa

Tanzania inatambulika kama kinara wa amani na usuluhishi tangu enzi za ukombozi wa nchi za kusini mwa Bara la Afrika na hivi karibuni katika utatuzi wa migogoro na ulinzi wa amani katika nchi za ukanda wa Maziwa Makuu. Tangu mwaka 2001, sera ya mambo ya nje ya Tanzania imejikita katika diplomasia ya kiuchumi. Sera hii itafanikiwa zaidi iwapo Tanzania itapanua wigo na kutumia vyema nafasi yake kama taifa lenye ushawishi kwa kuziunganisha dhana za uchumi, siasa na utamaduni katika medani ya kimataifa ili kujiimarisha kiuchumi.

Katika kufanya hivyo, Tanzania itaimarisha nafasi na ushawishi wake katika ushirikiano na mataifa rafiki, ndani ya jumuiya mbalimbali kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Nchi za Mwambao wa Bahari ya Hindi, nchi za Maziwa Makuu, na Umoja wa Afrika. Lengo ni kuhakikisha kuwa sera za kikanda zinaakisi na kulinda maslahi ya kiuchumi ya taifa, kuendeleza biashara na uwekezaji, na kuimarisha mchango wake katika kudumisha usalama na utulivu wa kikanda. Mafanikio haya yatajengwa juu ya ushawishi wa Tanzania unaotokana na historia yake ya kuchangia amani na maridhiano, pamoja na kutumia vyema fursa za kipekee za kijiografia, ikiwa katika eneo la kimkakati, na rasilimali asilia mbalimbali kama vile madini, bioanuai, vyanzo vikubwa vya maji safi, mifugo, na misitu. Katika muktadha huu, Tanzania itaendelea kuwa kiungo muhimu kati ya nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini, sambamba na kujiunganisha kwa ufanisi na masoko mapya yanayoibuka barani Asia na Amerika ya Kusini.

Hali hii itaweza kuvutia uwekezaji kutoka nje, hususan katika sekta zinazotegemea rasilimali na zinazovutia uwekezaji, kuhamasisha uhamishaji wa teknolojia, kuvutia wataalamu, na kupanua fursa za usafirishaji wa bidhaa nje, huku ikiongeza ushawishi wa Tanzania kwenye masuala muhimu ya kimataifa kama vile biashara, maendeleo endelevu, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Pia, Tanzania inadhamiria kunufaika na watanzania waishio ughaibuni na raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania kama fursa ya kuongeza mapato, mitaji na kutumia ujuzi na teknolojia walionayo.

Kwa kutumia urithi wake wa kiutamaduni wenye utajiri mkubwa, sekta ya sanaa, ubunifu na michezo inayokua kwa kasi, Kiswahili kama nyenzo ya diplomasia na lugha yenye manufaa ya kiuchumi inayopanuka na kutambulika kimataifa. Tanzania inatarajiwa kuongeza ushawishi wake na kuwa kivutio cha uwekezaji kutoka nje, kukuza utalii, na kuongeza ushirikiano katika kubadilishana maarifa na ujuzi.

Katika kufanikisha juhudi hizi, pia kuna umuhimu wa kuongeza umahiri wa lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kigeni ili kukuza weledi katika mawasiliano, kupanua fursa za Watanzania kimataifa, na kuimarisha ushindani wa Taifa katika medani za kimataifa.

***Matarajio***

a) Taifa linaloenzi urithi wake wa kihistoria katika ukombozi wa Bara la Afrika na kutumia vyema fursa za mabadiliko ulimwenguni ili kuongeza ushawishi wake kidiplomasia.

b) Taifa linaloongoza katika kudumisha utulivu na amani barani Afrika na duniani kote, na kuchangia kikamilifu kulinda haki za binadamu na juhudi za kupambana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi huku likitetea ipasavyo maslahi ya bara la Afrika.

c) Ushirikiano wa kimkakati na nchi zilizoendelea na zinazoendelea kiuchumi unaolenga kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kiuchumi, kwa lengo la kuvutia uwekezaji na maendeleo ya teknolojia.

d) Kuongeza ushawishi wa Tanzania kupitia nyanja za utamaduni kwa kukuza Kiswahili kama nyenzo ya kidiplomasia na lugha yenye manufaa ya kiuchumi katika ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa.

e) Jamii yenye uwezo wa kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kimataifa, inayoshiriki kikamilifu katika diplomasia ya kimataifa, biashara na ubunifu, ikichangia mustakabali mzuri wa Taifa.

# Nguzo ya Pili

## Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii



## 4.2. Nguzo ya Pili: Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

Watu wenye uwezo ni nguzo muhimu ya kufikia malengo ya Dira 2050. Uwezo wa watu na jamii unajumuisha ujuzi, stadi za maisha, uhuru wa kuchagua na kufanya maamuzi, pamoja na fursa zilizopo zinazomwezesha kila mtu kuishi maisha bora. Katika kujenga uwezo huu, ni muhimu kuwekeza katika malezi bora na makuzi ya watoto, elimu bora na mafunzo, huduma bora za afya, pamoja na mifumo imara na endelevu ya hifadhi ya jamii.

Dira 2050 inalenga kuimarisha uwezo wa watu na ustawi wa jamii, ikiwa na dhamira ya dhati katika kuleta usawa wa kijinsia kwa wote na kuwa na jamii jumuishi. Ili kufikia malengo haya, ni lazima kuwawezesha watu tangu utotoni hadi uzeeni, kwa kutumia mbinu thabiti zikiambatana na kudumisha maadili mema, kujenga hulka ya kujiamini na kujifunza bila ukomo.

Sambamba na hayo, ni muhimu kujenga jamii imara na jumuishi, yenye umoja na mshikamano na iliyo sawa bila kujali tofauti za kijamii na kimaeneo, na kuhakikisha makundi mbalimbali, yakiwemo ya wanawake, watu wenye ulemavu, na wale wanaoishi katika mazingira magumu, yanapata fursa na huduma muhimu.

Kwa kuwekeza kimkakati katika kujenga uwezo wa watu, hususan kwa watoto na vijana ambao ndiyo idadi kubwa ya jamii, pamoja na kuwawezesha wanawake na watu wenye ulemavu, Tanzania inaweza kujenga mazingira ambamo wananchi wote wanastawi. Mtazamo huu utajenga mfumo shirikishi na wenye misingi ya maadili, kuimarisha nguvukazi yenye ujuzi na ari, na kuendeleza jamii yenye mshikamano, utamaduni, na usawa kwa wote.

## Maeneo ya Kipaumbele

### 4.2.1 Jamii Iliyoelimika, yenye Ujuzi na Inayopenda Kujifunza

Elimu na ujuzi, kuanzia hatua za awali za malezi na makuzi ya mtoto, ni muhimu katika kujenga uwezo wa mtu kifikra na kiubunifu, na katika kufanya uchambuzi, kutatua changamoto, na kuwa na utaalamu na umahiri katika nyanja mbalimbali za maisha. Malezi bora na makuzi ya mtoto, elimu, ujuzi, na kujifunza pasipo ukomo, humjengea mtu uwezo wa kuhimili mabadiliko, jambo ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya kila mtu na Taifa kwa ujumla. Uwekezaji katika malezi na makuzi ya watoto pamoja na elimu bora ya awali ni nyenzo muhimu ya kuondoa umaskini, kuongeza ushiriki wa watu hususan wanawake katika uchumi na uongozi, kuchochea usawa wa kijinsia, na kuweka msingi thabiti wa maendeleo ya kielimu na kitaaluma kwa vizazi vijavyo.

Malezi na makuzi bora pamoja na fursa za elimu ya awali kwa watoto hadi kufikia umri wa miaka minane ni muhimu, kwani asilimia 90 ya ukuaji wa ubongo wa mwanadamu hutokea katika umri huu, hususan katika miaka mitano ya kwanza. Umri huu ndio hujenga msingi imara wa ukuaji kimwili, kiakili, kihisia na kijamii, mambo ambayo ni muhimu kwa ajili ya kujiendeleza kielimu na kufanikiwa kimaisha.

Tanzania inalenga kuwa na mfumo wa elimu jumuishi unaoandaa wananchi kwa ujuzi na maarifa yanayohitajika katika uchumi wa kisasa na kimataifa. Ili kuwajengea watoto na vijana uwezo wa kuchangia maendeleo ya uchumi unaoendeshwa na mabadiliko ya kiteknolojia, ni muhimu kuweka mkazo katika stadi za sayansi, teknolojia, uhandisi, na hisabati, pamoja na ujuzi wa kina wa kidijitali. Vilevile, stadi za maisha, elimu ya ujasiriamali, na usimamizi wa fedha zinahitajika ili kuwaandaa watoto na vijana kwa dunia inayobadilika, ikiwemo kupunguza pengo la ujuzi na kuimarisha usawa wa kijinsia. Kupitia mfumo jumuishi wa elimu na mafunzo, Tanzania inakusudia kujenga nguvukazi yenye ujuzi, uthabiti, na uwezo wa kuchochea maendeleo ya taifa.

Sekta ya elimu nchini imepiga hatua kubwa ikishuhudia uwekezaji katika miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, mafunzo ya ualimu, uboreshaji wa sera ya elimu na mafunzo na mitaala.

Licha ya mafanikio haya, ni muhumu kuendelea kuimarisha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia sambamba na ongezeko la idadi ya wanafunzi. Aidha, ni muhimu kuendelea kuboresha mfumo wa elimu na mafunzo nchini ili kuendana na mabadiliko ya wakati ili kuwaandaa wahitimu kukabiliana na ushindani katika dunia inayobadilika kwa kasi.

***Matarajio***

a) Taifa ambalo kila mtoto anapata malezi na makuzi bora, analindwa na anapata msingi imara wa kujifunza na wa maisha, kupitia vituo vya malezi na makuzi, pamoja na elimu bora na ya lazima ya awali, inayotolewa kupitia mfumo madhubuti na endelevu unaojitegemea.

b) Mfumo wa elimu na mafunzo bora, jumuishi, unaostahimili changamoto, wenye viwango vya ubora vinavyotambulika kimataifa, unaozalisha wahitimu wenye maarifa, ujuzi, na stadi za maisha pamoja na mtazamo chanya utakaowawezesha kuchangia katika maendeleo endelevu ya Taifa. Walimu na wakufunzi mahiri na wenye ari watakuwa nguzo muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji.

c) Shule na taasisi za elimu salama na jumuishi zinazoweka kipaumbele kwenye ustawi na fursa sawa kwa watoto na vijana wote.

d) Wahitimu wenye ujuzi stahiki na uwezo wa kushindana na kufanikiwa katika soko la ajira kimataifa.

e) Jamii bunifu na stahimilivu inayoongozwa na maarifa katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

f) Jamii yenye elimu na maarifa ya fedha ambapo watu wana uwezo wa kufanya maamuzi sahihi juu ya matumizi ya fedha, kusimamia rasilimali kwa ufanisi na kuchangia katika ukuaji wa uchumi.

g) Jamii inayojifunza bila kikomo kwa lengo la kujenga uwezo wa kila Mtanzania kukabiliana na mabadiliko ya kiulimwengu.

### 4.2.2 Jamii yenye Afya

Jamii yenye afya ni ile ambamo watu wanapata ustawi wa kimwili, kiakili na kijamii, ili kujenga taifa la watu wenye uwezo. Aidha, jamii yenye afya inahusisha upatikanaji wa huduma bora za afya na  mtindo wa maisha unaozingatia misingi ya afya inayokubalika.

Tanzania imeendelea kujenga jamii yenye afya kwa kuimarisha sekta ya afya hasa kuwekeza katika miundombinu ya kufikisha huduma za afya nchini kote pamoja na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, hususan katika maeneo ya vijijini. Aidha, kumekuwa na jitihada za ziada za kuongeza bajeti ya Serikali na kubuni mifumo ya bima ya afya kwa wote ili kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma za afya kwa gharama nafuu. Upatikanaji wa huduma za afya umeimarika ambapo kwa mujibu wa kipimo cha Afya kwa Wote cha Shirikia la Afya la Duniani, Tanzania imepanda kutoka alama 38 mwaka 2015 hadi 43 mwaka 2022. Aidha, programu zinazoendelea za kuzuia na kudhibiti magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza, magonjwa ya mlipuko, sambamba na kufuata utaratibu wa usimamizi wa huduma za afya ujulikanao kama “Afya Moja”, zinaakisi dhamira ya nchi katika kuboresha afya ya jamii.

Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo, kasi ya ongezeko la idadi ya watu ikiambatana na umaskini, athari za mabadiliko ya tabianchi, kuenea kwa magonjwa yasiyoambukiza na ya milipuko, vinaongeza changamoto kubwa katika sekta ya afya. Ili kukabiliana na changamoto hizi, ni muhimu kuimarisha sekta ya afya kwa kuongeza huduma za afya ya msingi, kwa lengo la kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana kwa wote na kwa gharama nafuu.

Maendeleo ya teknolojia ya kidijitali yanazidi kuboresha mfumo wa afya kwa njia za kisasa. Aidha, matumizi ya teknolojia yanarahisisha uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa na kuwezesha huduma kuwafikia wananchi karibu na maeneo yao na kwa muda mfupi. Dira 2050 inalenga kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za afya kwa kuimarisha mifumo ya afya inayotumia teknolojia ili kutoa huduma zenye ubora, nafuu na zinazopatikana kwa wote.

***Matarajio***

a) Kuwa na huduma bora za afya kwa wote, zenye mfumo wa uhakika na endelevu wa kugharamia na unaotoa kipaumbele kwa wanawake, watoto, vijana, wazee na watu wenye ulemavu.

b) Kuwa taifa la watu wenye ustahimilivu, na jamii iliyo tayari kuimarisha afya na kujikinga na maradhi kwa kuzingatia mtindo wa maisha unaowezesha kukabiliana na magonjwa ya milipuko, changamoto za afya na mabadiliko ya tabianchi.

c) Kuwa na jamii yenye afya ambapo kila mtu anapata huduma za afya kwa usawa na kwa gharama nafuu.

d) Kuwa na jamii ambayo kila mtu anastawi kutokana na lishe bora na analindwa dhidi ya bidhaa zenye madhara.

e) Kuwa kitovu cha kikanda katika uzalishaji wa bidhaa bora za afya na lishe, ili kuhakikisha bidhaa hizi zinapatikana kwa wingi na kwa gharama nafuu.

f) Kuwa kitovu cha huduma bobezi za afya, zinazokidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi na kuvutia utalii wa kimatibabu.

g) Kuwa na mfumo wa afya unaotumia teknolojia za kisasa kama vile akili unde katika kung'amua na kudhibiti maradhi kwenye vinasaba.

h) Kuwa na elimu na huduma bora za afya ya uzazi kwa wote.

i) Kuwa taifa ambalo hakuna mwanamke anayepoteza maisha wakati wa kujifungua na kila mtoto anayezaliwa anaishi na kustawi.

### 4.2.3 Hifadhi ya Jamii

Hifadhi ya jamii ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Ina lengo la kuhakikisha ustawi na usalama wa kijamii kwa watu na familia kutokana na hali mbalimbali kama vile uzee, ugonjwa, ajali au ukosefu wa ajira. Hifadhi ya jamii ina mchango muhimu hususan katika kupunguza pengo la usawa na kuboresha maisha ya watu. Mfumo wa hifadhi ya jamii unajumuisha jitihada za Serikali na wadau wengine ili kudhibiti, kusimamia na kupunguza hatari zinazoweza kutishia ustawi wa watu, kaya na jamii. Kwa muda mrefu jamii ya Tanzania kama zilivyo jamii nyingine za Kiafrika zimekuwa na utamaduni wa asili wa kutoa huduma kwa wazee, watu wenye mahitaji muhimu kupitia familia au jumuiya. Hivyo, utamaduni huu unaweza kuendelea kutumika pamoja na mifumo ya kisasa ya hifadhi ya jamii ambayo itaweza kuwa jumuishi na endelevu.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika hifadhi ya jamii jumuishi na usawa wa kijinsia kwa kuanzisha mikakati inayolenga kupunguza umaskini na kuboresha ustawi wa makundi yaliyosahaulika katika mifumo mingi ya kijamii wakiwemo wazee na watu wenye ulemavu. Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti katika kujumuisha sekta isiyo rasmi katika mfumo wa hifadhi ya jamii, ikitambua umuhimu wa sekta hii kwa uchumi wa nchi. Hatua hizi zinalenga kuongeza faida za hifadhi ya jamii kwa wafanyakazi waliopo katika sekta isiyo rasmi ili kuwajumuisha na kuchangia kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Vilevile, Serikali imejumuisha wananchi wasio na ajira kwa kuanzisha programu za kuwezesha makundi yasiyo na uwezo, zikiwemo kaya maskini, watu wenye ulemavu, wazee, wazazi wasio na uwezo wa kujikimu na watoto wenye mahitaji maalum.

Mfumo huu pia unahusisha uchangiaji wa lazima kwa watu wenye ajira ambapo mwajiri na mfanyakazi huchangia mfuko wa hifadhi ya jamii ambao husaidia usalama wa kipato kwa wanufaika baada ya kustaafu au nyakati za kutokuwa na shughuli za kiuchumi.

Licha ya mafanikio haya, wananchi wengi hususan walio kwenye sekta isiyo rasmi na waishio vijijini bado hawajaunganishwa na hifadhi ya jamii. Pia, ukosefu wa rasilimali fedha unazuia uendelevu wa mifumo isiyohitaji michango ya moja kwa moja, pamoja na changamoto za kiutawala na uelewa mdogo kwa umma vikidhoofisha ufanisi wake.

Dira 2050 inalenga kuanzisha na kuimarisha mfumo jumuishi wa hifadhi ya jamii unaotumia teknolojia ili kutoa huduma bora zenye ufanisi na zinazowafikia watu wote. Kuimarisha programu zinazozingatia ustawi wa mtoto na hifadhi ya jamii kutahakikisha kwamba makundi yenye uhitaji, yakiwemo ya watoto, wazee, na watu wenye ulemavu, yanapata msaada stahiki. Aidha, mifumo ya kisheria itaimarishwa ili kutokomeza ukatili, ubaguzi na ajira kwa watoto, sambamba na kuhamasisha mifumo jumuishi inayoheshimu utu na usawa. Kwa kutumia teknolojia za kidijitali na ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, Tanzania itajenga mfumo wa hifadhi ya jamii ulio thabiti, jumuishi na endelevu.

***Matarajio***

a) Taifa ambalo kila mtu hususan wanawake, watu wenye ulemavu na wazee wananufaika na mifumo ya hifadhi ya jamii iliyo thabiti, bunifu na endelevu.

b) Jamii salama dhidi ya ajira kwa watoto, ukatili, na ubaguzi, ambapo kila mtoto analelewa katika mazingira salama, yenye malezi bora na fursa za maendeleo ili aweze kustawi kikamilifu.

c) Jamii ambayo makundi maalum na yenye uhitaji yameunganishwa kupitia mifuko maalum ya hifadhi ya jamii inayohakikisha kuwepo kwa usalama wa kipato, upatikanaji wa huduma muhimu, na fursa za uwezeshaji kiuchumi.

d) Taifa linalolinda kikamilifu maslahi ya watu wenye ulemavu kwa kuhakikisha upatikanaji sawia wa miundombinu, huduma na fursa.

e) Jamii inayoundwa na familia imara ambazo zinawajibika na kushirikiana katika kuimarisha uadilifu, maadili na ustawi wa kila mtu.

#### 4.2.4 Makazi Bora ya Gharama Nafuu

Makazi bora ya gharama nafuu ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii, kiuchumi na mazingira. Ujenzi wa makazi bora ni pamoja na kuunganisha miundombinu ya huduma za kijamii kama vile nishati safi, maji safi na salama, barabara, miundombinu ya maji taka na taka ngumu, na utunzaji wa mazingira. Makazi bora yanasaidia katika kuchangia usalama, utulivu na ukuaji wa uchumi.

Makazi mijini yameendelea kukua kwa kasi, yakichochewa na ongezeko la idadi ya watu wanaohama kutoka vijijini kwenda mijini kwa ajili ya kutafuta fursa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Inakadiriwa kuwa, ifikapo mwaka 2050, zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania wataishi mijini. Ongezeko hilo la idadi ya watu mijini linaweza kusababisha ujenzi holela wa makazi, miundombinu duni ya usafiri wa umma na ya maji safi na salama, na uchafuzi wa mazingira endapo hatua muhimu hazitachukuliwa.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, ni muhimu kuwekeza katika maboresho ya miundombinu ya makazi na mipango miji. Muhimu pia ni ujenzi wa makazi nafuu na urasimishaji wa makazi yasiyo rasmi pamoja na kuweka mifumo ya usafiri katika miji inayokua kwa kasi. Aidha, msisitizo umewekwa katika maendeleo endelevu ya makazi, kupitia dhana ya “Miji ya Kijani na ya Kisasa” inayojumuisha matumizi ya nishati safi.

Makazi katika maeneo ya vijijini yanajumuisha nyumba za asili, ambapo nyingi hujengwa kwa udongo, miti au matofali ya udongo. Ni idadi ndogo tu ya nyumba hujengwa kwa matofali ya saruji au mawe na kuezekwa kwa mabati. Kuboresha makazi na huduma za kijamii vijijini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba bora, miundombinu ya barabara na upatikanaji wa nishati safi, maji safi na salama na usafi wa mazingira ni hatua muhimu za kuongeza fursa za kiuchumi na kijamii na hivyo kupunguza wimbi la wakazi wa vijijini kwenda mijini.

Dira 2050 inalenga kujenga makazi bora na ya gharama nafuu ili kuwa na taifa endelevu na lenye mafanikio kupitia mipango jumuishi ya kukuza uchumi, uvumbuzi wa kiteknolojia, uhifadhi wa mazingira na ustawi wa jamii.

***Matarajio***

a) Taifa ambalo kila mtu ana makazi bora na nafuu yanayochochea jamii endelevu mijini na vijijini.

b) Taifa lenye uwiano mzuri na jumuishi wa maendeleo kati ya miji, vijiji na kanda.

c) Miji endelevu ya kisasa na ya kijani inayochochea maisha yenye ustawi kwa wote, wakiwemo watu wenye ulemavu.

d) Taifa ambalo kila mtu anapata huduma nafuu za maji safi na salama sambamba na huduma bora za usafi wa mazingira ili kuimarisha afya ya jamii.

e) Mtandao imara wa nishati unaotoa kipaumbele kwa nishati safi na mbadala, ukipunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa, kulinda mazingira, na kuhakikisha upatikanaji wa nishati endelevu kwa sekta zote za jamii.

f) Taifa lenye mifumo bora ya usafiri wa umma, inayorahisisha usafiri wa watu na usafirishaji wa bidhaa.

### 4.2.5 Nguvukazi yenye Ujuzi na Ari

Nguvukazi yenye ujuzi na ari ni muhimu katika kufanikisha lengo la kufikia uchumi jumuishi wa kati ngazi ya juu. Ili kufikia lengo hilo, ni muhimu kuwa na nguvukazi yenye kujituma na yenye ubunifu inayotokana na mazingira ya kazi salama na yenye motisha.

Tanzania imeendeleza rasilimali watu kwa kuwekeza kwenye upatikanaji wa elimu bora na ujuzi, lishe, huduma za afya na hifadhi ya jamii. Pamoja na hayo, bado kuna changamoto kadhaa katika ubora wa nguvukazi. Kiwango hicho cha ubora wa nguvukazi ya Taifa ni 0.39 tu kwa mujibu wa Kipimo cha Rasilimali watu, ambacho ni chini ya wastani wa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara cha 0.4. Hii inamaanisha kwamba, watoto wanaozaliwa leo wataweza kufikia asilimia 39 tu ya uwezo wao wa uzalishaji wakiwa watu wazima. Hali hii inaashiria changamoto kubwa katika mifumo ya afya na elimu. Changamoto nyingine ni kutoshabihiana kwa ujuzi wa nguvukazi na mahitaji halisi ya soko la ajira. Aidha, kasi ya ongezeko la idadi ya watu, hususan kutokana na uzazi, inasababisha utegemezi mkubwa, na hivyo kuwa mzigo mzito kwa uchumi na huduma za kijamii. Idadi kubwa ya wategemezi inazidisha shinikizo katika mifumo ya elimu na afya, jambo linalosababisha upungufu katika rasilimali na ubora wa huduma. Pia, mwenendo huu wa kidemografia unachelewesha upatikanaji wa fursa za kiuchumi. Changamoto nyingine ni ukosefu mkubwa wa ajira miongoni mwa vijana, kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia na uhaba wa fursa kwa watu wenye ulemavu.

Kuelekea mwaka 2050, Taifa litahitaji nguvukazi yenye uwezo na ujuzi mseto, uwezo mkubwa wa kufikiri, weledi katika matumizi ya taarifa, kwa kuzingatia tamaduni mbalimbali na kushirikiana na wengine, pamoja na kutumia teknolojia za kisasa. Ili kwenda sambamba na mabadiliko haya, ni muhimu kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi na kubadilika kulingana na maendeleo ya teknolojia. Jitihada hizi zitajenga nguvukazi imara, bunifu, na inayoweza kuhimili mabadiliko, na hivyo kuweza kushindana katika soko la ajira la kimataifa ambalo msingi wake ni teknolojia. Aidha, uwekezaji wa kimkakati katika elimu na afya ya uzazi, hasa kwa vijana, wanawake na wasichana, ni muhimu kwa maendeleo endelevu. Kwa kukuza uwezo huu, tunaweza kuunda nguvukazi imara na yenye ubunifu na ujuzi anuwai, inayowawezesha watu kustawi katika mazingira ya kazi yanayoendeshwa kwa kiasi kikubwa na teknolojia.

***Matarajio***

a) Nguvukazi mahiri na yenye ujuzi, inayotumia teknolojia, inayoweza kuhimili mabadiliko na kuchochea ubunifu na ushindani katika masoko ya ndani na ya kimataifa.

b) Taifa linalovutia, kukuza, na kuhifadhi vipaji na utaalamu miongoni mwa raia na wageni, ili kujenga rasilimali watu kwa lengo la kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

c) Idadi ya watu ambayo uchumi unaweza kuhimili, ili kuwa na maisha bora kwa kila mtu.

d) Jamii yenye uwazi, inayothamini kujifunza kutoka kwa wengine, na inayokuza ushindani katika soko la ajira ili kujenga nguvukazi yenye ujuzi, tija, na ubunifu.

e) Nguvukazi yenye motisha na ari, inayofanya kazi kwa bidii, uadilifu na maadili ili kuchochea kasi ya maendeleo.

### 4.2.6 Jamii yenye Umoja, Mshikamano na Inayowajibika

Umoja, mshikamano na uwajibikaji ni nguzo muhimu katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii na kuleta maendeleo kwa pamoja, na hivyo kuharakisha maendeleo ya taifa. Hali hii inajitokeza pale ambapo wananchi wanashirikiana kwa dhati, bila kutenganishwa na tofauti za kijinsia, kidini au kikabila, na kila mmoja akiwa na jukumu lake katika kujenga taifa. Umoja unaleta nguvu, mshikamano huimarisha ushirikiano, na uwajibikaji unahakikisha kila mmoja anatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na uadilifu.

Tanzania inaendelea kujenga taifa lenye umoja, mshikamano na uwajibikaji, ambapo lugha ya Kiswahili imekuwa na nafasi kubwa katika kuhamasisha umoja na ushirikishwaji wa wananchi. Kama lugha ya Taifa, Kiswahili kimeunganisha makabila zaidi ya 120, kimeimarisha umoja na utambulisho wa kitaifa, na

kimeendelea kuwa msingi muhimu katika kukuza maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kukuza ushawishi wa kikanda.

Vilevile, katika kuendelea kujenga jamii yenye ushirikiano, mshikamano na uwajibikaji, Tanzania imeweka mkazo mkubwa katika elimu ya uraia ili kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji na uzalendo, pamoja na kuongeza miradi ya jamii ili kuchochea ushiriki na kujenga dhana ya umiliki wa shughuli za maendeleo. Aidha, jitihada za Taifa katika kuendeleza michezo na shughuli za kiutamaduni tangu umri mdogo zinachochea uzalendo na mshikamano wa kijamii. Juhudi hizi zinatoa fursa kwa vijana kuendeleza vipaji vyao na kujivunia utambulisho wa taifa.

Licha ya jitihada hizi, bado kuna dhana iliyojengeka katika jamii ya kutegemea Serikali kufanya shughuli zote za maendeleo, jambo linalodhoofisha wajibu na jukumu la ushiriki wa wananchi. Changamoto nyingine sugu ni kutokuthamini muda kama rasilimali muhimu kwa ajili ya maendeleo, pamoja na ukosefu wa utunzaji bora wa mazingira.

***Matarajio***


a) Taifa lenye umoja, mshikamano na linaloendeleza na kutumia kikamilifu vipaji vya watu wake katika sanaa, ubunifu, michezo, na burudani kama kielelezo cha utambulisho wake.

b) Raia wanaowajibika, wenye maadili na uzalendo na ambao wanashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya kijamii.

c) Jamii yenye fikra za kimaendeleo inayotambua muda na rasilimali kama mali adhimu na adimu, zinazopaswa kutumiwa kwa uadilifu ili kuchagiza maendeleo ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla kwa faida ya kizazi cha leo na vizazi vijavyo.

# Nguzo ya Tatu

## Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi



## 4.3 Nguzo ya Tatu: Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ni muhimu katika kufikia malengo ya Dira 2050. Tanzania imejaaliwa utajiri wa maliasili na wingi wa bioanuai zilizopo katika mifumo mbalimbali ya ikolojia, kama vile misitu, uoto wa savana, mito na fukwe za bahari, hivyo kuifanya nchi kuwa eneo muhimu sana la bioanuai duniani. Aidha, Tanzania ina ardhi yenye rutuba, rasilimali za baharini na fukwe, mito na maziwa, ambayo huchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Usimamizi madhubuti wa maliasili huwezesha uhifadhi endelevu wa mazingira, ambao ni muhimu katika kuendeleza huduma na manufaa kwa rasilimali zenyewe na watu.

Katika kufikia lengo la kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu ifikapo 2050, matumizi endelevu ya rasilimali hizi na usimamizi wake madhubuti ni muhimu. Uhifadhi wa mazingira unahusisha ulinzi wa bioanuai, usimamizi endelevu wa rasilimali maji, ardhioevu, matumizi sahihi ya ardhi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira. Mabadiliko ya tabianchi yanayodhihirishwa na ongezeko la joto, hali ya hewa isiyotabirika, na majanga yanayotokea mara kwa mara, yanatishia maendeleo endelevu ya nchi. Madhara ya mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na vipindi virefu vya ukame, mafuriko, na kupotea kwa bioanuai, ambayo moja kwa moja yanaathiri sekta zinazotegemea hali ya hewa katika uzalishaji, kama vile kilimo, uvuvi, maji na misitu.

Kukabiliana na changamoto hizi kunahitaji juhudi za pamoja katika kujenga ustahimilivu wa jamii ili ziweze kuendana na mabadiliko ya tabianchi na mazingira. Hatua muhimu ni pamoja na kuongeza uelewa wa jamii kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi, kuhamasisha matumizi bora ya rasilimali, na kuimarisha mikakati ya uhifadhi wa mazingira. Kwa kufanya hivyo, Tanzania italinda mazingira, kuendeleza uchumi na kuhakikisha ustawi wa wananchi wake kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Nguzo hii inalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi inayothamini, kulinda na kutumia rasimali zake za asili kwa uendelevu, kuhifadhi mazingira na kuwa na ustahimilivu wa kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Kwa kuwa na mikakati madhuburi ya kulinda mifumo ya ikolojia na kukuza ustahimilivu, Tanzania itakuwa ni nchi yenye maisha bora, usawa, na ustawi kwa watu wake na urithi wake wa asili.

## Maeneo ya Kipaumbele

### 4.3.1 Uhifadhi wa Bioanuai

Tanzania inajivunia kuwa na bioanuai ya kipekee, ikijumuisha uoto wa asili wa misitu, mikoko na nyasi, wanyamapori, na makazi ya viumbe hai wa majini. Vilevile, Tanzania ni nchi yenye aina mbalimbali za mimea na wanyamapori wa kipekee, ambao ni sehemu muhimu ya urithi wa asili ambao unachochea utoaji wa huduma muhimu kwa mazingira na jamii. Utajiri huu wa asili unalindwa kupitia maeneo ya uhifadhi kama vile hifadhi za taifa na misitu, mapori ya akiba, mapori tengefu, hifadhi ya bahari, na hifadhi za wanyamapori za jamii, ambazo ni mahsusi kwa ulinzi wa bioanuai na kuruhusu matumizi endelevu kwa manufaa ya jamii na Taifa kwa ujumla. Eneo la hifadhi linalolindwa kisheria ni takriban asilimia 32 ya ardhi yote, ambalo ni muhimu kwa uhifadhi wa bioanuai, kudhibiti hewa ukaa, na kupunguza uchafuzi wa mazingira, sambamba na kutunza rutuba kwa ajili ya ustawi wa watu na Taifa. Hii inachangia kwa kiasi kikubwa kulinda mazingira, kukuza kilimo endelevu, na kuhakikisha usalama wa chakula na maji kwa vizazi vijavyo.

Rasilimali hizi ni muhimu kwa uchumi, hususan katika sekta ya utalii wa wanyamapori na fukwe, ambayo inachangia takriban asilimia 25 ya mapato ya fedha za kigeni na kutoa mchango mkubwa katika pato la taifa na kuongeza ajira. Rasilimali za misitu zinachangia asilimia 2.5 ya pato la taifa na asilimia 5.9 ya biashara ya kimataifa. Hata hivyo, rasilimali hizi zinakumbwa na tishio kubwa linalotokana na kuongezeka kwa shughuli za watu, kama vile upanuzi wa miji na maeneo ya kilimo na ufugaji, uharibifu wa misitu, uwindaji na biashara haramu ya nyara za wanyamapori hasa meno ya tembo, pembe za faru na nyamapori. Changamoto nyingine ni kuenea kwa viumbe vamizi na mmomonyoko wa ardhi. Mambo haya yanachangia kwa kiasi kikubwa kupotea kwa bioanuai, na hivyo kuhitaji juhudi za haraka za uhifadhi na usimamizi endelevu ili kuhakikisha rasilimali hizi zinatunzwa kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Katika kuhifadhi rasilimali hizi, Tanzania imekuwa na sera, sheria, mikakati na kanuni zinazoweka kipaumbele ushirikishwaji katika ngazi zote, kuanzia ngazi ya jamii hadi jumuiya ya kimataifa. Vipaumbele hivi vinakwenda sambamba na makubaliano ya kimataifa kuhusu uhifadhi wa bioanuai, kulinda urithi, na kuchangia juhudi za uhifadhi. Uhifadhi wa bioanuai kwa miaka 25 ijayo na kuendelea unahitaji mikakati endelevu ya kukabiliana na hatari hizi na nyingine zinazojitokeza, pamoja na kuimarisha mipango ya uhifadhi kwa ajili ya uendelevu wa bioanuai kwa vizazi vijavyo.

***Matarajio***

a) Kuwa miongoni mwa nchi mahiri katika uhifadhi wa bioanuai, yenye mifumo bora ya ikolojia, ambapo aina mbalimbali za viumbe hai zinastawi katika makazi yao ya asili.

b) Taifa kinara kwa matumizi endelevu ya bioanuai kwa manufaa ya ustawi wa jamii na maendeleo ya kiuchumi kwa kizazi cha sasa na kijacho.

c) Taifa linalokokotoa vyema thamani ya rasilimali za bioanuai na maliasili za nchi ili zitumike kikamilifu kuchangia katika pato la taifa na maendeleo ya jamii.

### 4.3.2 Uhifadhi wa Ardhioevu na Vyanzo vya Maji

Rasilimali maji na ardhioevu ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kwani zinachangia katika kilimo, mifugo, uzalishaji wa umeme na matumizi majumbani na viwandani. Pia, zinasaidia kuhifadhi bioanuai na kudhibiti mmomonyoko wa ardhi. Ardhioevu zina uwezo wa kuhifadhi maji ya mvua kwa kuyatoa polepole kwenye mifumo ya mito, hivyo kudhibiti mzunguko wa maji, kupunguza mafuriko, na kuhakikisha upatikanaji wa maji wakati wa kiangazi. Tanzania ina takriban hekta milioni 2.7 za eneo lenye mito ya kudumu na ya msimu, ambayo imesambaa sehemu kubwa ya nchi. Asilimia 37 hadi 45 ya uzalishaji wa nishati ya umeme hutokana na maji. Aidha, idadi kubwa ya watu inategemea kuwepo kwa ardhioevu na maji kwa ajili ya shughuli za kijamii na kiuchumi kama vile kilimo na ufugaji.

Pamoja na umuhimu mkubwa wa maji na ardhioevu, rasilimali hizi zinakabiliwa na changamoto kubwa kutokana na uvamizi na kuongezeka kwa shughuli za kimaendeleo. Ardhioevu zinapungua kila siku kwa sababu ya kuongezeka kwa mahitaji ya maeneo ya kilimo na makazi. Kwa mfano, kukauka kwa ardhioevu ya Ihefu kumekuwa na athari kubwa kwa bonde la Usangu, Mto Ruaha, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na ikolojia ya Bonde la Rufiji. Matokeo yake ni kuathirika kwa vyanzo vya kuzalisha umeme wa maji katika mabwawa ya Mtera, Kidatu, na Julius Nyerere, jambo linaloweza kuathiri uzalishaji wa umeme na mifumo ya maisha inayotegemea maji katika maeneo hayo.

Ifikapo mwaka 2050, inakadiriwa kwamba Tanzania itakuwa na uhaba mkubwa wa maji kutokana na ongezeko la idadi ya watu, shughuli za kiuchumi na mabadiliko ya tabianchi. Ingawa mwaka 2022, upatikanaji wa maji nchini ulikuwa mita za ujazo 2,105 kwa mtu, ambayo ni zaidi ya kiwango cha wastani cha dunia cha mita za ujazo 1,700, upatikanaji wa maji kwa matumizi ya binadamu unaendelea kupungua. Hali hii inasababishwa na mvua zisizotabirika, uharibifu wa vyanzo vya maji, kuongezeka kwa mahitaji ya maji na usimamizi dhaifu wa rasilimali maji. Vilevile, Taifa linaendelea kukabiliwa na changamoto ya ubora wa maji kutokana na uchafuzi wa mazingira. Ili kujihakikishia maendeleo ya kijamii, kiuchumi na mazingira panahitajika usimamizi thabiti wa rasilimali maji na ardhioevu.

***Matarajio***

a) Ardhioevu bora zinazochangia ustawi wa watu, kukuza uchumi na kutoa huduma muhimu za kiikolojia.

b) Taifa lenye uhakika na usalama wa maji kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi na linalodumisha na kuendeleza uhifadhi wa ikolojia.

c) Taifa lenye mfumo imara na shirikishi wa usimamizi wa ardhioevu, maji na rasilimali nyinginezo.

### 4.3.3 Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira

Uchafuzi wa mazingira nchini ni changamoto inayoendelea kuongezeka, hususan katika maeneo yenye idadi kubwa ya watu kama vile majiji na miji. Uchafuzi huu una athari kubwa kwa afya ya jamii, ustawi wa uchumi na mazingira kwa ujumla. Changamoto hizi zinatokana na vyanzo mbalimbali, ikiwemo moshi wa magari, shughuli za viwanda, uchomaji wa taka, matumizi makubwa ya mbolea za kemikali na viuatilifu, kelele, pamoja na utupaji holela wa taka na ukosefu wa mifumo madhubuti ya usimamizi wa taka.

Moshi kutoka katika mitambo, vyombo vya moto, na viwanda unachangia kwa kiasi kikubwa katika matatizo ya kiafya kama magonjwa ya moyo na mfumo wa kupumua. Aidha, kelele zinazozidi viwango vya kawaida kutokana na shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi katikati ya makazi watu husababisha msongo wa mawazo na matatizo ya kusikia. Uharibifu wa ardhi unahatarisha uzalishaji wa mazao na usalama wa chakula, unaosababishwa na matumizi makubwa na yasiyo endelevu ya mbolea zenye kemikali na dawa za kilimo, pamoja na miundombinu duni na chakavu ya usimamizi wa taka. Vilevile, majitaka kutoka viwandani na majumbani yasiyochakatwa husababisha uchafuzi mkubwa wa maji, uharibifu wa ikolojia, na kudhoofisha mifumo ya maisha ya viumbe hai, hali ambayo inaathiri moja kwa moja ustawi wa jamii.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ni muhimu kwa kulinda afya ya jamii, mazingira, na maendeleo ya uchumi. Tanzania imechukua hatua anuwai zikiwemo kutunga sera, sheria na mikakati mbalimbali ili kupambana na uchafuzi wa mazingira na kuimarisha utunzaji endelevu wa mazingira. Hatua hizi zinajumuisha kushirikisha jamii, sekta binafsi, na taasisi za serikali katika kulinda mazingira kwa kizazi cha sasa na kijacho. Licha ya juhudi za kuboresha huduma za usimamizi wa taka na miundombinu, mifumo hii haiendani na ongezeko kubwa la taka linalotokana na ongezeko la shughuli za kijamii na kiuchumi. Hivyo, hatua madhubuti zinahitajika kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za mazingira kwa maendeleo jumuishi na ustawi wa taifa.

***Matarajio***

a) Jamii yenye uelewa mkubwa wa athari za uchafuzi wa mazingira ili kuwa na mazingira salama na endelevu kwa wote.

b) Majiji na miji yenye miundombinu na usimamizi bora wa taka na ujenzi unaozingatia uhifadhi wa mazingira.

c) Taifa kinara katika matumizi endelevu ya rasilimali na linalotumia taka kama malighafi kwa manufaa ya kiuchumi.

d) Taifa lenye mazingira stahimilivu linalosimamia vyema maliasili kwa maendeleo ya uchumi wa kijani.

#### 4.3.4 Usimamizi Madhubuti wa Ardhi

Ardhi ni rasilimali muhimu inayotoa fursa kwa ajili ya maendeleo ya kilimo, viwanda, makazi na shughuli nyingine za kiuchumi. Tanzania ina takriban kilomita za mraba 1,000,000 za ardhi, ambayo ni muhimu kwa maendeleo endelevu. Pamoja na ukubwa huu wa ardhi, kasi ya ongezeko la watu, ukuaji wa miji, upanuzi wa shughuli za kilimo, uchimbaji madini na maendeleo ya viwanda vinaongeza mahitaji ya ardhi. Kwa upande mwingine, mfumo wa kisheria uliopo, pamoja na mila na desturi za kijamii, umeendeleza hali ya kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limekuwa kikwazo kwa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu katika kupata na kumiliki ardhi kwa haki na usawa. Urasimu katika upatikanaji wa nyaraka za umiliki wa ardhi, kutokuwa na mipango thabiti ya matumizi ya ardhi, migogoro ya mipaka ya vijiji, makazi yasiyo rasmi, uhaba wa nyumba na ongezeko la migogoro ya matumizi ya ardhi ni miongoni mwa mambo yanayokwamisha usimamizi wa ardhi. Changamoto nyingine zinazochangia usimamizi hafifu wa ardhi ni pamoja na uhaba wa fedha na rasilimali watu, mapungufu ya kiteknolojia na kukosekana kwa mfumo imara wa uratibu.

Ili kushughulikia changamoto hizo, Tanzania imeweka miongozo ya kisera inayolenga kuimarisha usimamizi wa ardhi, ikiwemo kurasimisha umiliki wa ardhi, matumizi endelevu ya ardhi na kushirikisha jamii katika usimamizi wa maliasili. Katika siku zijazo, juhudi za pamoja na makusudi zitahitajika ili kuweka uwiano wa malengo ya uhifadhi na shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kwa ajili ya kuhakikisha rasilimali ardhi inatumika kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

***Matarajio***

a) Nchi iliyopangwa vizuri na kuweka wazi matumizi ya ardhi, yakiwemo ya makazi, kilimo, mifugo, viwanda na hifadhi.

b) Usimamizi bora wa ardhi unaoongozwa na nguvu ya soko la ardhi, mali isiyohamishika na huduma, ili kuvutia uwekezaji unaotegemea ardhi.

c) Jamii yenye usawa ambapo kila mwananchi, hususan wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, wanapata fursa sawia za umiliki wa ardhi.

d) Taifa ambalo mipaka imepimwa kwa usahihi, kuimarishwa kikamilifu na inayotambulika kimataifa.

### 4.3.5 Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Katika miongo ya hivi karibuni, Tanzania imekumbwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, kama inavyodhihirika kupitia ongezeko la joto na mvua zisizotabirika, mambo ambayo yanaathiri shughuli za kijamii na kiuchumi. Mabadiliko haya kwa kiasi kikubwa yanatokana na uzalishaji wa hewa ya ukaa. Tangu mwaka 1980 pamekuwa na ongezeko kubwa la joto ardhini na baharini. Makadirio yanaonesha kuwa ifikapo mwaka 2041, maeneo ya kanda ya magharibi na kati yatashuhudia ongezeko la joto la zaidi ya nyuzi joto mbili, huku maeneo ya mashariki yakitarajiwa kuongezeka kwa nyuzi joto moja. Kuongezeka kwa joto kunatishia usalama wa chakula kwa kupunguza uzalishaji wa kilimo na kuleta hatari kubwa za kiafya, ambapo ongezeko la nyuzi joto moja linahusishwa na ongezeko la asilimia 15–29 la maambukizi ya kipindupindu na kuenea kwa magonjwa yanayoambukiza kama vile homa ya matumbo na kuhara.

Kuanzia miaka ya 1970 kumekuwa na mabadiliko ya viwango vya mvua ambayo yamesababababisha uhaba wa maji kwa baadhi ya maeneo, ongezeko la mafuriko, moto wa nyika, kuharibika kwa miundombinu na kuongezeka kwa viumbe na mimea vamizi, pamoja na uharibifu wa matumbawe na bioanuai. Mabadiliko haya pia yameongeza kuwepo kwa mazalia ya vimelea vya magonjwa kama vile malaria na homa ya dengue. Bila kuchukua hatua thabiti, mabadiliko ya tabianchi yanaweza kudhoofisha ukuaji wa uchumi na kuushusha hadi asilimia nne ifikapo mwaka 2050, na hivyo kuwaingiza watu milioni 2.6 katika umaskini, huku watu milioni 13 wakilazimika kuhama kwenye makazi yao.

Katika kushughulikia changamoto hizo Serikali imefanya jitihada za kuboresha sera na taasisi na kutumia fursa zinazojitokeza kimataifa katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, bado kunakosekana urasimishaji wa kutosha wa sera miongoni mwa taasisi za utekelezaji, jambo linalopelekea vikwazo katika uratibu na utekelezaji. Wanawake, watoto na watu wenye ulemavu wamekuwa wahanga wakubwa wa athari za mabadiliko ya tabianchi.

Changamoto hizi zinahitaji hatua za haraka ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kulinda mifumo ya ikolojia na kuhakikisha ustawi wa jamii.

***Matarajio***

a) Taifa endelevu na stahimilivu linalotumia nishati safi na ya gharama nafuu na linalosimamia kwa ufanisi uzalishaji wa hewa ukaa kwa ajili ya mustakabali wa nchi.

b) Taifa lenye uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, likilinda wananchi wake, miundombinu na mali dhidi ya majanga ya asili na yale yatokanayo na shughuli za kibinadamu, ambapo wanawake na vijana wapo mstari wa mbele.

c) Taifa kinara katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, likiwa ni kielelezo katika ustahimilivu, uendelevu, na uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

d) Taifa linalotumia kikamilifu fursa za biashara ya hewa ukaa na upatikanaji wa fedha kupitia ajenda ya mabadiliko ya tabianchi duniani ili kuongeza uwezo wa jamii na taifa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.


Vichocheo

# 5. VICHOCHEO VYA KUFIKIA MALENGO YA DIRA

Vichocheo vya maendeleo ni nyenzo muhimu katika kuongeza kasi ya kufikia malengo ya Dira 2050. Dira hii imebainisha vichocheo vitano vya maendeleo - usafirishaji fungamanishi, nishati, sayansi na teknolojia, utafiti na maendeleo na mageuzi ya kidijitali. Usafirishaji fungamanishi unaimarisha uratibu na usimamizi wa mtiririko wa bidhaa, huduma, taarifa na rasilimali kupitia mnyororo wa usambazaji, kuanzia kwenye uzalishaji hadi kwa mtumiaji wa mwisho, kwa ufanisi na kwa gharama nafuu. Nishati ya uhakika ni nyenzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya viwanda na shughuli mbalimbali za kiuchumi, ili kuboresha viwango vya maisha kwa kutoa fursa za ajira kwa maendeleo endelevu katika jamii. Sayansi na Teknolojia zinachochea ubunifu na hivyo kuongeza tija na ushindani. Eneo la utafiti na maendeleo ni kichocheo muhimu cha kuongeza maarifa yatakayoibua bidhaa na huduma mpya kwa ajili ya kutatua changamoto za kiuchumi na kijamii na kuongeza kasi ya maendeleo. Mageuzi ya kidijitali yatachangia kwa kiasi kikubwa matumizi ya teknolojia bunifu, kuboresha utoaji wa huduma, kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za uzalishaji na kuimarisha utendaji kazi. Kwa pamoja, vichocheo hivi vitakuwa na mchango mkubwa katika kuongeza kasi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kuongeza uzalishaji, na kuboresha hali ya maisha ya wananchi, na hatimaye kufanikisha malengo ya Dira 2050.

## 5.1. Usafirishaji Fungamanishi

Usafirishaji fungamanishi unajumuisha mfumo mzima wa usafirishaji wa bidhaa, utoaji wa huduma, shughuli za watu, na upatikanaji wa taarifa. Hii inahitaji ushirikiano thabiti kati ya usafirishaji, wadau wa uzalishaji, uhifadhi, usambazaji na utoaji wa huduma ili kuongeza ufanisi, kuimarisha mifumo na kupunguza gharama. Wakati Tanzania ikidhamiria kufanya mageuzi makubwa ya kiuchumi, kuimarisha mfumo wa usafirishaji ni hatua muhimu kwa maendeleo endelevu.

Katika miaka ya hivi karibuni, Tanzania imepiga hatua kubwa katika sekta ya usafirishaji kwa kuwekeza katika miundombinu ya kimkakati, kufanya mageuzi ya kimuundo na kuimarisha matumizi ya teknolojia, huku ikitumia ipasavyo nafasi yake ya kijiografia kama lango la biashara kwa Afrika Mashariki na Kusini. Hatua hizo ni pamoja na uwekezaji katika mtandao wa barabara, reli ya kisasa ya SGR na upanuzi wa bandari na viwanja vya ndege. Kadhalika, Serikali imeboresha utendaji wa Shirika la Ndege la Tanzania, ikiwemo ununuzi wa ndege za kisasa na kuongeza safari za ndani na nje.

Uwekezaji huu umeimarisha miundombinu ya usafirishaji ndani ya nchi na pia kuiunganisha Tanzania na nchi jirani, na hivyo kukuza biashara za kikanda na ushirikiano wa kiuchumi. Aidha, kuanzishwa kwa vituo vya huduma za pamoja mipakani kumeimarisha biashara mipakani, huku matumizi ya teknolojia za kidijitali yakiboresha usimamizi wa kodi na vibali, udhibiti wa hesabu, ufuatiliaji wa mizigo na ufanisi katika mfumo wote wa usambazaji. Kwa ujumla, maendeleo haya yanaifanya Tanzania kuwa kitovu muhimu cha usafirishaji katika ukanda wa Afrika mashariki, kati na kusini, hivyo kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi na kukuza ushindani wa kibiashara.

Licha ya jitihada hizi, bado vikwazo katika biashara ya kusafirisha mizigo vipo. Gharama za usafirishaji pekee zinachangia kati ya asilimia 35 na 45 ya gharama zote za kuagiza bidhaa kutoka nje, vikiwemo bima na usafiri. Hali hii inaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zenye gharama kubwa zaidi za uingizaji wa mizigo duniani. Kadhalika, kuna kiwango kikubwa cha ucheleweshaji wa kupakua na kusafirisha mizigo kutokana na uhaba wa vifaa, maghala na mtandao wa usafirishaji usio imara. Pamoja na haya, mfumo wa sheria na taratibu za usafirishaji una changamoto nyingi, kama vile udhibiti wa kukithiri na utitiri wa kodi na sheria nyingine ndogo ndogo za serikali za mitaa zinazokinzana na sheria kuu za nchi. Kutatua changamoto hizi ni muhimu katika kuboresha sekta ya usafirishaji, kuchochea ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira na kuifanya Tanzania kuwa na ushindani mkubwa zaidi katika biashara za kikanda na kimataifa.

***Matarajio***

a) Tanzania kuwa lango kuu la biashara mashariki na kusini mwa Afrika ikitumia nafasi yake ya kijiografia kurahisisha biashara mipakani na kuimarisha ushirikiano.

b) Taifa linaloongoza kwa biashara ya usafirishaji likiunganisha nchi za Afrika Mashariki, za kati na kusini na masoko mengine ya kimataifa.

c) Mtandao wa usafirishaji fungamanishi wenye mfumo wa kisasa na shindani, unaounganisha shoroba za kiuchumi ili kuwezesha biashara za ndani na za kimataifa kwa ufanisi na kuongeza ushindani wa Tanzania katika sekta ya usafirishaji.

d) Watoa huduma za usafirishaji wenye viwango vya kimataifa, wenye kutoa huduma kwa ushindani huku wakitumia teknolojia za kisasa za kidijitali ili kuongeza ufanisi na kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa katika mnyororo wa thamani.

e) Mazingira bora ya usimamizi wa usafirishaji yanayorahisisha taratibu za forodha, kupunguza urasimu na vikwazo, kuzingatia viwango vya kimataifa, na kuendana na kasi ya maendeleo katika sekta ya usafirishaji.

f) Mtandao jumuishi wa usafirishaji wenye miundombinu inayozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu ili kutoa fursa sawa kwa wote katika biashara za ndani na kimataifa.

## 5.2. Nishati

Upatikanaji wa nishati ya uhakika ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii. Umuhimu wa nishati unajidhihirisha kuanzia matumizi ya kila siku majumbani na ofisini hadi katika sekta za viwandani na mifumo ya usafirishaji. Nishati ina mchango mkubwa kwenye kuboresha viwango vya maisha na kuinua ustawi wa jamii, na hivyo kuleta maendeleo endelevu kwa taifa. Tafiti zinaonesha kuwa umeme ni nyenzo muhimu katika kuwatoa watu katika umaskini, sambamba na elimu na kiwango stahimilivu cha ongezeko la idadi ya watu.

Tanzania imepiga hatua kwenye sekta ya nishati, ambapo matumizi ya nishati ya umeme kwa kila mtu yameongezeka kufikia wastani wa 170 kWh na yanatarajiwa kuongezeka na kufikia 3,000 kWh ifikapo mwaka 2050. Baadhi ya jitihada zinazoendelea katika kuimarisha sekta ya nishati ni uwekezaji mkubwa unaolenga kupanua uwezo wa kuzalisha nishati endelevu na ya kuaminika ikiwemo nishati ya maji, jua, upepo, nyuklia na jotoardhi. Mfano halisi wa juhudi hizi ni mradi wa kuzalisha umeme wa Bwawa la Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115. Juhudi zinaendelea kupunguza upotevu wa nishati wakati wa usambazaji kutoka asilimia 16 hadi chini ya 10. Hatua hii inajumuisha uboreshaji wa miundombinu ya usambazaji ili kuhakikisha mfumo wa usafirishaji wa nishati unakuwa imara na wenye ufanisi zaidi.

Licha ya maendeleo haya, sekta ya nishati bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo miundombinu isiyokidhi mahitaji, usimamizi usioridhisha wa sheria za nishati na upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya kuboresha upatikanaji wa nishati ya uhakika. Kukabiliana na changamoto hizi kunahitaji juhudi za pamoja ili kuhakikisha uthabiti wa sera, kujenga uwezo wa kiufundi na kuimarisha ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya kuongeza ufanisi na uendelevu.

***Matarajio***

a) Mfumo bora wa nishati safi ulio stahimilivu, wenye ufanisi, wa kuaminika na wa gharama nafuu.

b) Miundombinu thabiti ya nishati inayochochea maendeleo ya viwanda na ustawi wa kiuchumi na kijamii.

c) Taifa linalozalisha nishati ya kutosha kukidhi mahitaji ya ndani, huku likijipambanua kuwa moja ya wazalishaji wakuu wa nishati katika ukanda wa mashariki na kusini mwa Afrika.

## 5.3. Sayansi na Teknolojia

Kasi ya mabadiliko ya kiuchumi na kijamii duniani inategemea maarifa. Sayansi na teknolojia ni vichocheo muhimu vinavyoleta tija, ufanisi na ukuaji endelevu wa uchumi. Tanzania imepiga hatua katika matumizi ya teknolojia kwenye sekta mbalimbali, ikilenga kuongeza ufanisi, kuboresha upatikanaji wa huduma na kuimarisha uzalishaji. Hatua hizo ni pamoja na uwekezaji katika sekta ya nishati, yakiwemo matumizi ya nishati mbadala ya jua na bayogesi, ili kukidhi mahitaji na kuongeza kasi ya maendeleo hasa vijijini. Kwa upande mwingine, bayoteknolojia imeendelea kutumika kwa upana katika sekta za kilimo, utalii, madini, mifugo, elimu, afya na viwanda, ikilenga kuongeza uwezo wa uzalishaji, ufanisi, kupunguza gharama na kuimarisha ushindani wa kiuchumi, kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi.

Kwa ujumla, Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuweka mazingira wezeshi kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia ili kukidhi mahitaji ya jamii. Hatua hizi ni pamoja na kutoa kipaumbele kwa masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati katika ngazi zote za elimu. Licha ya juhudi hizo, bado kuna mapungufu, kama vile ukosefu wa miundombinu, upungufu wa fedha, ukosefu wa ujuzi wa kutosha kulingana na mahitaji, ushirikiano mdogo baina ya wadau, na kutokuwa na mipango thabiti inayorahisisha uingizaji wa teknolojia kutoka nchi zilizoendelea. Aidha, kukosekana kwa usawa katika upatikanaji wa elimu bora kwa masomo ya hisabati, sayansi, na teknolojia baina ya wanawake na wanaume pamoja na kutokuwepo jitihada madhubuti zinazolenga ugunduzi wa mapema wa vipaji kwa watoto, ni changamoto nyingine zinazokwamisha upatikanaji wa ujuzi stahiki kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia. Wakati jitihada za kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia zikiendelea, tayari kuna mjadala mkubwa kuhusu jinsi ya kwenda sambamba na maendeleo ya akili unde na teknolojia nyingine bila kuathiri maadili katika jamii. Tanzania itaendelea kuharakisha matumizi ya teknolojia za kisasa kwa lengo la kuchochea maendeleo. Hii ni pamoja na uwekezaji makini katika nishati mbadala ili kuongeza upatikanaji wa nishati mbadala na endelevu na uwekezaji kwenye bayoteknolojia kwa ajili ya kuongeza tija katika kilimo, viwanda na afya.

Kwa kutumia kikamilifu nguvu ya mageuzi ya sayansi na teknolojia, Tanzania inalenga kuwa taifa lenye uwezo mkubwa wa kiteknolojia, lenye ustahimilivu, linalohamasisha maendeleo endelevu na kuboresha maisha ya watu kwa mustakabali wa usawa na ustawi.

***Matarajio***

a) Ongezeko kubwa la matumizi ya teknolojia za kisasa katika ngazi zote za uzalishaji na utoaji wa huduma ili kuongeza ufanisi na kuchochea mabadiliko.

b) Kuwa na vituo vya ubunifu na maeneo mahususi yenye hadhi ya kimataifa kwa ajili ya tafiti na uvumbuzi katika sekta muhimu kama kilimo, viwanda na afya, vikiwa na wataalamu mahiri na rasilimali za kutosha kukidhi mahitaji ya viwanda vya ndani.

c) Jamii inayotumia teknolojia za kisasa zinazojumuisha na kukidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu, kwa kuzingatia mifumo inayowapa fursa ya kushiriki kikamilifu na kuchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

d) Taasisi imara zinazofanya ufuatiliaji na tathmini ya taarifa za maendeleo ya kiteknolojia ili kuiandaa nchi kuwa tayari kutumia teknolojia kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kuimarisha ushindani.

e) Mfumo jumuishi unaokuza masomo na matumizi ya sayansi, teknolojia, uhandisi, na hisabati, ukiwa na lengo la kutoa fursa sawa na kuwawezesha wanawake na wasichana kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kisayansi na ubunifu.

f) Uwekezaji thabiti na jumuishi katika kukuza na kutumia teknolojia zinazoibuka ili kusaidia viwanda na kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

## 5.4. Utafiti na Maendeleo

Kadri nchi inavyoendelea, Utafiti na Maendeleo ni nyenzo muhimu katika kuongeza ubunifu, kutatua changamoto za ndani, na kuongeza tija katika uzalishaji. Vilevile, utafiti na maendeleo huimarisha ukuzaji wa ustadi, husaidia kutoa mwongozo wa uundaji wa sera, na kukuza mbinu endelevu za maendeleo, hivyo kuimarisha ushindani wa nchi katika soko la kimataifa.

Kwa kutambua umuhimu huu, Serikali imechukua hatua madhubuti za kuongeza kasi ya utafiti, ikiwa ni pamoja na kuongeza bajeti ya utafiti, kuimarisha ushirikiano baina ya vyuo vikuu, taasisi za utafiti na sekta za uzalishaji na huduma, sambamba na kuongeza juhudi za kuhamasisha maendeleo na matumizi ya teknolojia bunifu.

Hatua hizi zimechochea ongezeko la kiwango cha ubunifu, ambalo linadhihirishwa na kuongezeka kwa kampuni zinazochipukia, vituo vya ubunifu, vituo vya kulea na kustawisha mawazo ya biashara na programu za ukuzaji wa biashara. Aidha, taasisi za elimu nchini zimeongeza mkazo kwenye Utafiti na Maendeleo, sambamba na kuimarisha mifumo ya kulinda hakimiliki, jambo linalosaidia kuhifadhi haki za wabunifu na kukuza utamaduni wa ubunifu na uvumbuzi. Licha ya maendeleo haya, bado kuna athari kwenye matumizi ya utafiti, ikiwemo uhaba wa fedha, miundombinu isiyotosheleza na ushirikiano mdogo baina ya wadau. Vilevile, changamoto za kisheria, upungufu wa wataalamu kutokana na kuhama kwa nguvukazi, uelewa mdogo wa umma na tofauti za kijinsia zinaendelea kukwamisha ukuaji wa shughuli za utafiti na maendeleo.

***Matarajio***

a) Mfumo imara wa utafiti na maendeleo unaovutia ushirikiano wa kimataifa, ukiimarishwa na ulinzi madhubuti wa hakimiliki ili kuchochea ubunifu na kuendeleza uwekezaji.

b) Mfumo wa uhakika wa kugharamia utafiti na maendeleo, kwa kutumia kiwango kisichopungua asilimia moja ya Pato la Taifa, na unaotoa motisha kwa sekta binafsi kuwekeza katika sekta muhimu kama kilimo, bioteknolojia, nishati safi na teknolojia zinazoibukia katika TEHAMA na nyanja nyingine.

c) Taifa lenye mtazamo wa kimaendeleo na lenye utamaduni wa kufanya maamuzi kwa kutegemea ushahidi wa kisayansi, likichochewa na utafiti wa kiwango cha hali ya juu ili kuimarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

d) Kitovu cha ubunifu cha kikanda kinachochochea uvumbuzi kwa wataalamu wa ndani na kinachotoa huduma kamili za ubunifu, kuanzia uvumbuzi hadi kufanya biashara.

e) Vyuo vya elimu ya juu na taasisi mahiri za utafiti zenye viwango vya kimataifa, na zenye ushirikiano thabiti na sekta mbalimbali kwa ajili ya kuchochea ubunifu kwenye uzalishaji na kutatua changamoto za jamii.

f) Mfumo imara wa kuendeleza ubunifu unaoendana na maendeleo ya kiteknolojia, utakaoifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa uvumbuzi duniani.

## 5.5. Mageuzi ya Kidijitali

Mageuzi ya kidijitali ni kichocheo muhimu cha maendeleo katika karne ya 21. Kuelekea mwaka 2050, kuna fursa kubwa ya kuharakisha maendeleo kupitia teknolojia za kidijitali ili kufikia malengo ya Dira 2050 kwa kuboresha ukuaji wa uchumi na kuimarisha huduma za kijamii. Kwa kutumia teknolojia hizi kwa ufanisi, Tanzania itaongeza ushindani wake, itapanua wigo wa uchumi na huduma, kuboresha uwezo wa kufanya maamuzi, kuongeza huduma jumuishi za kifedha, kuendeleza matumizi ya huduma za kidijitali katika sekta mbalimbali na kujenga uwezo wa kutumia teknolojia mpya zinazoibuka.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya teknolojia za kidijitali, ikidhihirishwa na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za kifedha kupitia simu za mkononi, upatikanaji wa intaneti yenye kasi na maendeleo ya serikali mtandao ambayo kwa kiasi kikubwa yameboresha utoaji wa huduma kwa umma. Huduma za kifedha kupitia simu za mkononi zimeleta mapinduzi kwenye sekta ya fedha ambapo sehemu kubwa ya jamii imeweza kupata huduma za kibenki kupitia simu za mkononi, jambo ambalo limesaidia watu wengi hasa waishio vijijini. Aidha, teknolojia za kidijitali zimeleta mabadiliko katika utoaji wa huduma za afya, elimu na kilimo na hivyo kuongeza ufanisi katika utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kuibuka kwa vituo vya ubunifu na ongezeko la kampuni zinazochipukia zinazojihusisha na masuala ya teknolojia kunadhihirisha dhamira ya dhati ya nchi ya kuongeza matumizi ya teknolojia za kidijitali kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Aidha, kumekuwepo jitihada kubwa katika usimamizi wa taarifa ili kusaidia kufanya maamuzi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma. Jitihada hizo ni pamoja na kuanzishwa kwa mifumo ya kitaasisi ya usimamizi wa taarifa na uwekezaji katika miundombinu ya taarifa, kama vile uanzishwaji wa vituo vya kuhifadhi na kulinda taarifa.

Pamoja na mafanikio haya, maendeleo na mageuzi ya kidijitali nchini bado yanahitaji juhudi za ziada kwenye maeneo kadhaa - miundombinu, usalama wa kimtandao, gharama kubwa, uwezo mdogo wa watumiaji na vikwazo vya kisheria katika usambazaji na matumizi ya teknolojia. Pia kuna upatikanaji wa teknolojia kwa wananchi, hususan maeneo ya vijijini, pamoja na uwekezaji na matumizi madogo ya teknolojia zinazoibuka kama vile akili unde, *blockchain* na *internet of things*. Aidha, kumekuwa na ongezeko la wasiwasi kuhusu ukosefu wa uwiano kati ya maendeleo na maadili katika matumizi ya teknolojia mpya, hususan teknolojia za akili unde. Ili kushughulikia changamoto hizi na kuhakikisha kwamba manufaa yake yanawafikia watu kwa kiwango kikubwa, itakuwa muhimu kuwekeza katika rasilimali watu, miundombinu na sera madhubuti zitakazosaidia kutumia teknolojia hizi kuharakisha maendeleo.

***Matarajio***

a) Jamii yenye umahiri katika matumizi salama ya mitandao na teknolojia za kidijitali, na inayozingatia misingi bora na maadili kwa maslahi ya jamii na taifa.

b) Kitovu cha kikanda cha maendeleo ya teknolojia kinachohamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa ili kuendeleza ubunifu, kuchochea maendeleo na kuongeza ushindani wake katika soko la kimataifa.

c) Upatikanaji wa intaneti ya kasi na huduma za mawasiliano zilizo na uhakika na za gharama nafuu kote nchini.

d) Mfumo thabiti na jumuishi wa usimamizi wa takwimu na taarifa unaowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi, za kuaminika na kwa wakati, huku taifa likidumisha mamlaka kamili ya kudhibiti, kuhifadhi na kutumia taarifa hizo kwa mujibu wa sheria na maslahi ya kitaifa.

e) Ongezeko la matumizi ya data kibiashara kwa lengo la kuongeza thamani yake kiuchumi na kuongeza ajira.

f) Taifa linaloongoza katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini kwa uzalishaji wa programu za kompyuta na maudhui ya kidijitali, kwa matumizi ya soko la ndani na la kimataifa.

g) Taifa lililo mstari wa mbele katika matumizi ya teknolojia zinazoibukia, lenye nguvukazi yenye mtazamo wa kisasa ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

h) Serikali mtandao inayotoa huduma bora, jumuishi, na zenye ufanisi kwa raia na biashara, kwa lengo la kuimarisha ubora wa huduma za Serikali.

# 6. SEKTA ZA MAGEUZI

Wakati Tanzania inaelekea kutimiza malengo yake ya maendeleo, ni muhimu kuainisha sekta zenye uwezo mkubwa wa kuleta mageuzi ya haraka ya kiuchumi, kijamii na kimazingira. Sekta hizi zina uwezo mkubwa wa kukua, kuongeza fursa za ajira na ubunifu, na kuchochea shughuli za uzalishaji na huduma ambazo ni muhimu kwa masoko ya ndani na nje. Pamoja na utajiri wake wa rasilimali na fursa, Tanzania ipo katika nafasi nzuri ya kutumia kikamilfu fursa zitokanazo na sekta hizi na hivyo, kuongeza ubora wa maisha na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi.

Ili kutumia rasilimali za Taifa kwa ufanisi katika kufanikisha malengo ya maendeleo, Dira 2050 inatoa mwongozo wa kuweka vigezo vya kuchagua na kutoa kipaumbele kwa sekta zenye uwezo mkubwa wa kuchochea mageuzi ya kijamii na kiuchumi. Dira hii inaweka msingi thabiti wa kuchagua sekta za kipaumbele zitakazochangia kuleta mageuzi ya kweli katika uchumi na ustawi wa wananchi. Aidha, mwongozo huu unatambua umuhimu wa mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia katika kuliandaa Taifa kukabiliana na changamoto zinazoibuka na kutumia ipasavyo fursa mpya kwa maendeleo endelevu na jumuishi.



## 6.1 VIGEZO VYA UCHAGUZI WA SEKTA

Dira 2050 imeainisha vigezo vya kuchagua sekta za mageuzi. Sekta zitachaguliwa kwa kuzingatia uwezo wa sekta hiyo katika:

1. **Kuzalisha ajira kwa wingi**
   Sekta ya kipaumbele iwe na uwezo wa kuzalisha ajira yenyewe na kuchochea uzalishaji wa ajira katika sekta nyingine.
2. **Kuongeza mauzo ya nje**
   Sekta iwe na uwezo wa kuuza bidhaa na huduma zinazohitajika katika masoko ya nje, na yenye uwezo wa kuunganisha soko la ndani na la nje.
3. **Kukua yenyewe na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine**
   Sekta ya kipaumbele iwe na uwezo wa kukua yenyewe na kuchochea ukuaji na uzalishaji wa sekta nyingine.
4. **Kuongeza thamani**
   Kipaumbele kitaelekezwa kwenye sekta ambazo inatoa fursa kwa malighafi nabidhaa kuongezwa thamani kabla ya kumfikia mtumiaji.
5. **Kukuza mapato ya Serikali**
   Sekta iwe na uwezo wa kuzalisha na kukuza vyanzo vya mapato kwa wingi na kwa muda mrefu.

## 6.2 BAADHI YA SEKTA ZENYE FURSA ZA MAGEUZI KUELEKEA 2050

Kwa kuzingatia vigezo vya hapo juu, sekta zifuatazo zimebainishwa kuwa na uwezo mkubwa wa kuchochea kufikiwa kwa malengo ya Dira 2050.

i. **Sekta ya kilimo** inayojumuisha mazao, mifugo, uvuvi na misitu, bado ni mhimili wa uchumi wa Tanzania, ikichangia asilimia 26.5 ya pato la Taifa, ikiajiri asilimia 65 ya nguvukazi na kuzalisha asilimia 30 ya mapato ya mauzo ya nje. Sekta hii ina uwezo wa kuzalisha ajira nyingi na kuchochea ongezeko la mapato kupitia mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani. Uhusiano wake na sekta za viwanda, usafirishaji na biashara unabainisha nafasi yake katika kukuza ajira na uchumi.

   Katika siku zijazo, kilimo kitaendelea kuwa nguzo ya uchumi wa Tanzania. Kufikia mwaka 2050, sekta hii inatarajiwa kuwa na mabadiliko makubwa, yenye tija, endelevu na yenye ushindani wa hali ya juu. Hii itaifanya Tanzania kuwa kitovu cha chakula katika ukanda wa Afrika. Mageuzi yanahitajika katika kila sekta ndogo ya kilimo: sekta ya mazao itaweka mkazo kwenye mazao yenye thamani kubwa sokoni;

sekta ya mifugo itaboreshwa kwa kuwekeza katika uzalishaji wa kisasa wa bidhaa zinazotokana na mifugo kwa kuongeza tija na thamani ili kukidhi mahitaji ya masoko ya ndani na nje; sekta ya uvuvi itaimarishwa kwa kuendeleza uvuvi na ufugaji wa samaki, usimamizi wa mazao ya uvuvi na miundombinu baridi ya uhifadhi na usafirishaji; na sekta ya misitu inahitaji mikakati thabiti ya uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu, pamoja na kuendeleza biashara ya mazao ya misitu na upandaji wa miti kibiashara.

Mafanikio ya mageuzi ya sekta ya kilimo yatahitaji uwekezaji mkubwa katika teknolojia ya kisasa, miundombinu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na programu za kuwawezesha wakulima kukuza biashara zao. Vilevile, ni muhimu kuwekeza katika nishati nafuu, upatikanaji wa fedha, upanuzi wa mitandao ya masoko na kuhimiza mbinu endelevu za kilimo. Mikakati hii kwa pamoja itasaidia kujenga sekta ya kilimo iliyo imara, jumuishi, na yenye ushindani wa kimataifa, sekta itakayoweka msingi wa ustawi wa kijamii na kiuchumi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

ii. **Sekta ya utalii**, ambayo unachangia asilimia 25 ya mapato ya mauzo ya nje ya Tanzania, ni mojawapo ya sekta kuu za uchumi. Sekta hii ina mchango muhimu katika kuimarisha urari wa malipo na kuchochea ukuaji wa pato la Taifa. Utalii unaendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ya fedha za kigeni, ukichochea sekta muhimu kama vile za ukarimu, usafiri na biashara. Kuongezeka kwa idadi ya watalii wa nje na ndani kunathibitisha taathira chanya kwa uchumi, huku sekta hiyo ikichochea maendeleo jumuishi na endelevu.

Kufikia mwaka 2050, utalii unatarajiwa kuwa moja ya vyanzo vikuu vya ajira za moja kwa moja na zinginezo huku fursa kubwa zikionekana katika sekta za ukarimu, kuongoza watalii, usafirishaji na biashara za ndani. Sekta hii itapanuka zaidi na kuvutia wageni wa nje na ndani kupitia utalii unaohusisha utamaduni, urithi wa asili na malikale, utalii endelevu wa mazingira, utalii wa meli na fukwe, utalii wa uwindaji na wa mikutano na maonesho, na hivyo kuongeza mapato ya fedha za kigeni. Ukuaji huu utategemea uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu, utangazaji katika masoko lengwa na ushirikishwaji wa jamii katika maeneo mbalimbali ya utalii. Ni muhimu kukuza utamaduni wa kutoa huduma bora ili kuimarisha ushindani wa utalii wa Tanzania. Kupitia hatua hizi, Tanzania inalenga kuwa kitovu cha utalii barani Afrika ifikapo mwaka 2050.

iii. **Sekta ya uzalishaji viwandani** nchini Tanzania itapanuka na kuwa msingi wa ukuaji wa uchumi ifikapo mwaka 2050. Kwa muda mrefu kilimo kimekuwa uti wa mgongo wa uchumi wa nchi. Hata hivyo, kuitegemea sekta ya kilimo pekee kwa muda mrefu ni changamoto

kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi, kuyumba kwa bei, na misukosuko ya masoko duniani kunaweza kuiathiri nchi endapo sekta hii pekee inayotegemewa itayumba. Kwa upande mwingine, upanuzi wa sekta ya viwanda na uzalishaji utapunguza hatari hizi, utakuza uchumi na kuongeza uhimilivu wa mitikisiko ya nje. Kwa sasa, sekta ya viwanda inachangia asilimia 8.1 ya pato la Taifa na inakua kwa asilimia 8 kwa mwaka. Hivyo, ina uwezo mkubwa wa kuwa na taathira chanya katika sekta nyingine kama vile usindikaji wa mazao na uzalishaji wa vifaa vya ujenzi. Hii itaongeza thamani ya ndani, itapunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kuboresha uzalishaji wa mauzo ya nje.

Tanzania inalenga kuwa kitovu cha viwanda chenye ushindani kimataifa ifikapo mwaka 2050, ikitumia ongezeko la idadi ya watu, maendeleo ya kiteknolojia na msingi wake imara wa kilimo, kama nyenzo muhimu. Ili kufanikisha azma hii, ni muhimu kuimarisha miundombinu, kuboresha mazingira wezeshi ya biashara, kuimarisha sera, kujenga ujuzi wa rasilimali watu na kupanua wigo wa upatikanaji wa mitaji. Hatua hizi zitavutia uwekezaji wa ndani na nje, kuongeza tija, kusafirisha malighafi na pia kuzalisha bidhaa zilizokamilika na zilizoongezwa thamani.

iv. **Sekta za ujenzi na milki** zitakuwa kiini cha ukuaji wa miji ya Tanzania, zikikidhi mahitaji yanayoongezeka ya makazi, miundombinu, na huduma za umma, huku zikitengeneza fursa kubwa za kiuchumi. Kuelekea mwaka 2050, sekta ya ujenzi inatarajiwa kukua kwa kasi, ikizalisha mamilioni ya ajira katika nyanja za ujenzi, usanifu, uhandisi na kazi za ustadi. Ukuaji huu utachochea mapato na kuimarisha maendeleo ya miji yenye uwezo wa kukabiliana na changamoto za kisasa. Sekta hizi mbili zitafungamana na sekta za viwanda na huduma kama vile usimamizi wa mali na huduma za sheria. Ukuaji endelevu wa sekta hizi utatokana na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya kisasa, ujenzi wa makazi nafuu na mbinu endelevu za ujenzi.

v. **Sekta ya madini** ni mojawapo ya sekta muhimu zenye fursa kubwa ya kuchangia maendeleo ya nchi. Hii inatokana na utajiri wa rasilimali za madini, zikiwemo dhahabu, almasi, tanzanite, na madini ya kimkakati kama grafiti, lithiamu, urani, na madini adimu. Madini haya yanazidi kupata umuhimu na thamani kubwa wakati ambapo sekta ya nishati duniani inabadilika kuelekea nishati safi na kutumia teknolojia ambazo zinachangia uhifadhi wa mazingira. Katika miongo ijayo, sekta ya madini itakuwa na mchango mkubwa katika kukuza pato la Taifa, kufungua fursa za ajira, kuongeza mauzo ya nje na kuhaulisha teknolojia ya madini, huku ikichochea ukuaji wa sekta nyingine kama vile za ujenzi, viwanda, na nishati. Ili kupata manufaa ya muda mrefu kutokana na sekta hii, itakuwa muhimu kuwa na mbinu endelevu za uchimbaji madini, kanuni za wazi za usimamizi na uwekezaji katika teknolojia muafaka. Kuanzisha

viwanda vya kuongeza thamani ya madini kutasaidia kuzalisha ajira na kuongeza mapato ya mauzo ya nje, hivyo kuimarisha mchango wa sekta hii kwa uchumi wa Taifa.

vi. **Sekta ya uchumi wa buluu** unaozingatia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na maji baridi, utakuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo nchini. Tanzania, ambayo ina ukanda mrefu wa pwani, maziwa na mito mikubwa, ina fursa nyingi za kukuza sekta za uvuvi, utalii wa pwani na wa maziwa, usafiri wa majini, na matumizi ya nishati mbadala kutoka baharini. Sekta hizi zina nafasi kubwa ya kuongeza ajira, kukuza mapato, na kuhifadhi mazingira. Ili nchi iweze kutumia fursa hizi kikamilifu, itakuwa muhimu kuwekeza katika gesi asilia, uhifadhi wa bahari, uvuvi endelevu na ujenzi wa miundombinu. Hatua za kimkakati katika gesi asilia, uendelezaji wa bandari na upanuzi wa nishati ya kutumia maji zitachangia mpango madhubuti wa kutumia kikamilifu fursa za uchumi wa buluu Tanzania.

vii. **Sekta ya michezo na ubunifu** zina uwezo mkubwa ambao haujatumiwa kikamilifu katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Sekta hizi zinatoa fursa muhimu za ajira, kuendeleza ujuzi, kuwa chanzo cha kipato na kuwawezesha vijana, wakati huo huo zikijenga umoja na mshikamano wa jamii. Tanzania inalenga kuwa kitovu cha utamaduni, sanaa bunifu na michezo barani Afrika ifikapo mwaka 2050, ikiwa na sekta zinazostawi katika muziki, filamu, mitindo, na burudani. Kwa kukuza vipaji na kuweka mazingira wezeshi, Tanzania itafungua milango ya ubunifu na ujasiriamali kwa vijana. Kadhalika, uwekezaji kwenye mifumo ya haki za uvumbuzi utakuwa muhimu ili kuhakikisha kwamba sekta hizi zinashamiri na kuwa endelevu.

viii. **Sekta ya fedha** itakuwa kichocheo muhimu cha mageuzi ya kiuchumi Tanzania ifikapo mwaka 2050. Mahitaji ya huduma za kifedha, bima na uwekezaji yatakua kwa kiasi kikubwa kutokana na ongezeko la watu na ukuaji wa miji. Huduma bora za kifedha zitaimarisha upatikanaji wa mikopo, kukuza uwekezaji, kuweka akiba, na kuimarisha mbinu za ujasiriamali na hivyo kurasimisha shughuli za kiuchumi. Ili kunufaika na huduma hizi, ni muhimu kufanya mabadiliko ya sera, sheria na kanuni mbalimbali, kuboresha miundombinu ya kidijitali na kupunguza gharama za kupata mikopo. Kwa muktadha huu, lengo la Tanzania kuelekea 2050 ni kuwa na mfumo jumuishi wa fedha ambao utachangia kukua kwa uchumi.

ix. **Sekta ya huduma** itachukua nafasi muhimu katika kuendesha maendeleo ya Tanzania, hususan katika maeneo ya biashara, huduma za ukarimu, na huduma nyingine za kijamii na kiuchumi. Kuongezeka kwa watu walio na kipato cha kati kutaongeza mahitaji ya bidhaa na huduma, hivyo kuchochea ajira, kupanua fursa za biashara na kuimarisha shughuli za kiuchumi. Ili kutumia kikamilifu fursa hizi, Tanzania italazimika kuwekeza katika mafunzo, miundombinu, majukwaa ya kidijitali, na kuweka kanuni za kuwalinda watumiaji na kuhakikisha kwamba kunakuwa na ushindani kwa manufaa ya watumiaji.

# 7. MFUMO WA UTEKELEZAJI WA DIRA

Ili kuhakikisha Dira 2050 inatekelezwa kwa ufanisi, Serikali imeweka mfumo imara wa usimamizi unaozingatia malengo yake mahsusi. Mfumo huu umekusudia kuhimiza uwajibikaji, ukihitaji uongozi mahiri na ulio makini katika ufuatiliaji. Aidha, mfumo unahimiza matumizi ya mbinu zinazotoa matokeo yanayopimika.

Msingi wa mkakati huu ni mabadiliko makubwa ya kifikra - yakilenga vitendo badala ya maneno na matokeo badala ya ahadi. Uongozi, taasisi, pamoja na watendaji na wadau wote, wanapaswa kuwajibika ili kutimiza malengo ya Dira kwa ufanisi. Taasisi imara na mifumo madhubuti inayolenga kuondoa uzembe, inayohimiza uwajibikaji na kuchochea ufanisi itakuwa nguzo kuu za utekelezaji wa Dira 2050. Dira imeweka mfumo madhubuti wa utawala unaohakikisha utekelezaji unafanyika kwa nidhamu, sera zinasomana, taasisi zinakuwa imara na sekta na wadau wote wanashirikiana.

Ili kupunguza utegemezi wa misaada toka nje, mfumo wa utekelezaji utaweka mikakati maalum ya kuchagiza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, kukuza utamaduni wa kuweka akiba na matumizi mazuri ya rasilimali. Tanzania italazimika kujijenga kama taifa linalojitegemea kiuchumi likiongozwa na uwekezaji wa kimkakati. Hivyo, Dira 2050 inabainisha hatua muhimu zitakazoleta utekelezaji wenye ufanisi, kwa kuainisha vipaumbele, utekelezaji wa awamu, uratibu thabiti wa taasisi, na mfumo madhubuti unaozingatia matumizi ya takwimu ili kupima maendeleo katika kila hatua.

## 7.1 Kuweka Vipaumbele Kimkakati

Kwa kuzingatia uchache wa rasilimali zilizopo na malengo mapana ya Dira 2050, ni lazima kuweka vipaumbele kimkakati. Hivyo Dira hii imeweka utaratibu maalum wa kuchagua sekta kuu za mageuzi zitakazochochea mabadiliko ya kijamii na kiuchumi kwa haraka. Vigezo vya kuchagua sekta za mageuzi vinajumuisha uwezo wa sekta kuzalisha ajira nyingi, kuongeza mauzo ya nje na kukuza pato la taifa. Vigezo vingine ni sekta inayoweza kuchochea ukuaji wa sekta nyingine na kuongeza thamani ya bidhaa. Mkakati huu wa kuweka vipaumbele una lengo la kuhakikisha kunakuwa na uwiano kati ya ukuaji wa haraka wa uchumi na malengo ya muda mrefu ya kuijumuisha jamii, na kuwa na maendeleo endelevu na uhimilivu wa kiuchumi. Mkakati utahakikisha kwamba rasilimali zinaelekezwa kwenye maeneo yatakayoleta matokeo chanya na endelevu.

## 7.2 Mipango ya Utekelezaji wa Dira

Utekelezaji wa Dira 2050 utaongozwa na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa miaka 25. Mpango huu utatumika kama mwongozo wa kuandaa mipango ya maendeleo ya miaka mitano-mitano na mipango ya mwaka mmoja-mmoja. Utaratibu huu utahakikisha uendelevu wa mipango ya maendeleo, na kwenda sambamba na mabadiliko yanayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji.

## 7.3 Ushiriki wa Wadau

Mafanikio ya Dira 2050 yanategemea ushirikiano thabiti kati ya wadau mbalimbali. Ubia madhubuti kati ya sekta ya umma na binafsi ni nguzo muhimu za kuimarisha maendeleo endelevu, kwa kuunganisha uongozi wa serikali, ubunifu wa sekta binafsi, ushiriki wa asasi za kiraia, na ushirikishwaji wa wananchi kwa pamoja. Ushirikiano wa kimkakati kati ya watunga sera, wawekezaji, na jamii utaimarisha uratibu na kuhakikisha malengo ya kitaifa yanatimizwa kwa ufanisi.

## 7.4 Uratibu wa Utekelezaji

Ufanisi wa Dira 2050 unategemea uratibu thabiti na usimamizi utakaohakikisha kwamba Dira inatekelezwa kimkakati na inajibu changamoto zinazojitokeza. Ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi na asasi za kiraia ni muhimu katika kufikia maendeleo endelevu.

Tume ya Taifa ya Mipango, ikiwa ndiyo chombo kikuu cha uratibu wa mipango ya maendeleo, itakuwa na jukumu la kuhakikisha ushirikiano madhubuti kati ya wadau mbalimbali, kupanga kimkakati, na kuweka matumizi bora ya rasilimali. Kwa kushirikiana na Tume ya Mipango Zanzibar na wadau wengine, Tume ya Taifa ya Mipango itatumia mbinu shirikishi katika kuratibu utekelezaji wa Dira 2050, kuhakikisha sera na mipango ya kisekta vinafungamanishwa kikamilifu na malengo ya Dira pamoja na mipango ya maendeleo kwa ujumla. Hatua hizi zinalenga kutafsiri kwa ufanisi malengo ya Dira, kuongeza tija katika matumizi ya rasilimali, na kuimarisha usimamizi na maamuzi ya kimkakati kwa maendeleo jumuishi na endelevu ya taifa.

## 7.5 Ufuatiliaji, Tathmini na Uwajibikaji

Ili Dira 2050 iweze kuleta mabadiliko ya kweli, utekelezaji wake lazima ujikite katika mikakati inayotegemea taarifa za kitafiti ili kuwezesha maamuzi sahihi, matumizi bora ya rasilimali na uwajibikaji. Mfumo madhubuti wa kitaifa wa takwimu utakaounganisha takwimu za sekta mbalimbali utasaidia kuimarisha maamuzi. Uchambuzi wa kina wa mwenendo wa idadi ya watu, uchumi, upatikanaji wa rasilimali, na tofauti za kikanda, utatoa taswira ya mipango ya maendeleo na mikakati ya kisekta inayohitajika kwa wakati husika. Mbinu hii itahakikisha usawa, uwekezaji wenye tija, unaoijumuisha jamii na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi.

Mfumo wa kidijitali wa Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza utawezesha utekelezaji himilivu, utakaokabili misukosuko ya kiuchumi, mabadiliko ya tabianchi na maendeleo ya kiteknolojia. Matumizi ya teknolojia zinazoendelea kama vile akili unde, mifumo ya taarifa za kijiografia, na uchambuzi wa data kwa wakati halisi, yataleta ufanisi wa sera, ufuatiliaji, na mgawanyo wa rasilimali.

Ili kuimarisha uwajibikaji, viashiria vya utendaji vitatumika kufuatilia maendeleo, kutambua changamoto na kuboresha utendaji. Mfumo wa motisha na adhabu utaimarisha utamaduni wa uwajibikaji, ukihamasisha ubora na kuondoa uzembe na kuhakikisha kuwa utekelezaji unaleta matokeo yenye manufaa.

# 8. MWELEKEO

Dira 2050 inaweka mwelekeo thabiti wa mageuzi kuelekea Tanzania jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea. Dira hii inaakisi maono ya muda mrefu ya kitaifa ya kulinda na kuenzi haki za kikatiba, utu wa mwanadamu, amani, umoja wa kitaifa, demokrasia na ulinzi utunzaji wa rasilimali za nchi. Inatoa mwongozo wa kimkakati kwa safari ya taifa kuelekea ustawi wa kweli wa kijamii na kiuchumi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Mafanikio ya Dira 2050 yanategemea mshikamano wa dhati wa kila Mtanzania. Dira hii si ya serikali peke yake, bali ni mali ya kila mwananchi. Inahimiza ushirikiano mpana, ikitambua kuwa maendeleo ya kweli hujengwa kwa nguvu ya pamoja. Wanawake, vijana, na nguvukazi yenye ujuzi ni rasilimali ya kipekee yenye uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa. Ikiongozwa na mtazamo sahihi, ubunifu na uthubutu, nguvukazi hii itakabiliana na changamoto zozote, na kutumia fursa zinazojitokeza zikichagizwa na maendeleo ya kiteknolojia. Kwa kuweka mbele usawa wa kijinsia, elimu bora, na uwezeshaji wa vijana, Tanzania itajenga jamii iliyo thabiti, yenye usawa na maendeleo shirikishi.

Ushirikiano madhubuti kati ya sekta ya umma na binafsi ni msingi wa kufanikisha azma ya Dira. Kwa kuimarisha mshikamano, kuweka vipaumbele vya kimkakati, na kudumisha uwajibikaji wa hali ya juu, taifa litatimiza kwa mafanikio azma ya Dira 2050. Dira 2050 si tu ni mpango wa maendeleo, bali pia ni wito wa kizalendo kwa kila Mtanzania kushiriki katika ujenzi wa taifa linalojali watu wake, linalotoa fursa kwa wote, na linalotazama mbele kwa matumaini. Mustakabali wetu uko mikononi mwetu, tuungane kuijenga Tanzania ya haki, umoja na maendeleo endelevu kwa wote.

TUME YA TAIFA YA MIPANGO

NPC

Ustawi wa Pamoja

ISBN 978-9912-43-001-3

9 789912 430013